

**GUARDIOLA ADOKEZA KUONDOKA MAN CITY** UK. 22

Jumanne Mei 21, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581683

MWANGA WA JAMII

LIKE & FOLLOW US
www.twitter.com/nipashetz
www.ippmedia.com
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper

SHAMBULIO LA RISASI

# Familia ya Lissu yamdai haki AG



• **Mwenyewe** aahidi kulihamishia Makumbusho gari lenye matundu ya risasi, nguo alizovaa... *Uk. 2*



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akisikiliza maelezo kutoka kwa Christopher Kedendula wa Kampuni ya Swahili Honey ambao ni wazalishaji wa asali na watengenezaji wa mitambo ya kuchakata asali wakati wa ukaguzi wa mabanda ya maonesho katika Maadhimisho ya Siku ya Nyuki Duniani yaliyofanyika kitaifa ukumbi wa Jakaya Kikwete mkoani Dodoma jana. **PICHA: OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# Askofu 'aliyejinyonga' azikwa kikanisa, ripoti ya polisi yasubiriwa

UK. 2



UKURASA WA 4



**Waziri** aonya wanasiasa wanaogeuza jeshi mtaji wao

UKURASA WA 5

**Mbunge** aanika 'kisa na mkasa' vijana kutopiga kura uchaguzi



UKURASA WA 19



**Makamu** Rais Iran kurithi uongozi wa nchi siku 50

## Wanafunzi 486 kati ya 1,182 shuleni waketi sakafuni

UKURASA 5

**MICHEZO** YANGA YAANDAA 'SURPRISE' ZA UBINGWA UK.24

**KATUNI** UK.6

# Familia ya Lissu yamdai haki AG

**Elizabeth Zaya na Jenifer Gilla**

NGUO zenye damu ya Tundu Lissu pamoja na gari lake lenye matundu ya risasi vinapelekwa Makumbusho ya Taifa, familia ya Makamu Mwenyekiti huyo wa CHADEMA Tanzania Bara sasa inataka haki kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG).

Ijumaa iliyopita, Jeshi la Polisi Mkoa wa Dodoma lilimkabidhi Lissu gari lake aina ya Toyota Landcsruiser V8, VXR lililolishikilia tangu Septemba 7, 2017 aliposhambuliwa kwa risasi akiwa ndani ya gari hilo.

Kukiwa na mpango huo wa kulihamishia Makumbusho ya Taifa gari hilo, familia ya Lissu inaona hatua ya polisi kukabidhi gari hilo haitoshi; inataka vyombo vya sheria vitimize wajibu wake kwa kuwasaka na kuwatia hatiani waliohusika na shambulio hilo.

Kaka wa Lissu, Alute Lissu, akizungumza kwa niaba ya ndugu zake jana jijini kwao jimboni Singida Mashariki, alisema wao kama familia pamoja na Watanzania wengine, wanataka haki itendeke na hawatachoka kutafuta haki hiyo.

Ni kauli ya familia yao iliyotolewa baada ya Lissu kwenda kijijini kwao kuonesha gari hilo ikiwa ni siku chache baada ya kukabidhiwa na Jeshi la Polisi.

"Sisi kama ukoo bado tunalia kwamba haki itendeke, kuhakikisha wale watu waliotaka kuchukua maisha ya Lissu kabla ya muda wake, wasakwe na kupelekwa mbele ya sheria ili waadhibiwe kwa sababu wamefanya jambo la uovu kabisa.

"Kwa hiyo, tutaendela kusisitiza na kutaka kufahamu na ninafikiri siyo sisi peke yetu, ni pamoja Watanzania. Kwa ujumla wao wanatamani kujua ni nini na nani waliotaka kuondoa uhai wa huyu ndugu yetu.

"Mtanzania huyu ambaye ni sawa na Mtanzania yeyote, ana haki ya kuishi au kufa uzeeni, ana haki ya kupakata wajukuu zake, si kukatishwa maisha katikati halafu lisitokee jambo lolote," alisema.

Alute alisema ni lazima kuwe na uwajibikaji wa vyombo vyenye jukumu hilo kujua kitu gani kilitokea, kwa sababu gani na hatua iliyofikiwa katika upelelezi wa polisi kwa waliotaka kumuua. Alisisitiza wanayo haki ya kufahamu hilo.

Kaka huyo wa Lissu alieleza kuwa mdogo wake aposhambuliwa na kupelekwa Nairobi, Kenya kwa ajili ya matibabu ya kibingwa, alifuatilia kutafuta haki ikiwamo kwa Jeshi la Polisi na kutaka kufanyike uchunguzi wa kina, hali kadhalika kwa AG kuwasilisha hoja hiyo hiyo.

"Labda niseme kwamba ndugu yangu huyu alipopatwa na shambulio na kupelekwa Nairobi kwa ajili ya matibabu, mimi na ndugu zangu tulikuwa tunafuatilia mambo yake na kumsemea na katika kumsemea tulikuwa tunataka polisi wafanye uchunguzi wa kina ili kufahamu wahalifu ni kina nani na wamechukuliwa hatua gani.

"Tulichukua hatua mpaka kuandika barua kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na baada ya kusubiri mwezi mmoja, hatukuona kitu chochote, tulimwomba AG aombe nchi za kirafiki walete mpelelezi kutoka huko ili aje afanye upelelezi huru.

"Hatuwezi kuchoka kudai haki hii na kesi za jinai hazina ukomo. Tuna haki na Watanzania wana haki ya kujua kilichotokea ili waovu wasitawale, maana tukikaa kimya tukiwa waoga ndivyo waovu wanatawala na hatuwezi kukubali waovu watawale kwa kweli," alisema.



Alieleza kuwa wao familia wanataka gari alilokuwamo ndugu yao wakati anashambuliwa pamoja na nguo zake alizokuwa amevaa wakati wa tukio, vitumike kama kumbukumbu.

"(Familia) tunafikiria kuwa pamoja na kwamba fedha hatuna, lakini (Lissu) angalie uwezekano wa kutafuta gari lingine, hili libaki kama kumbukumbu ya Septemba 7, mwaka 2017 aliposhambuliwa.

"Kwa hiyo, tunaomba ulitunze, nguo iliyokuwa na damu siku umepigwa risasi na viatu utunze, usitupe wala usifue, kuonesha kwamba waovu hawashindi, wanaweza kushinda kwa muda mfupi lakini uovu haulipi," alitamka akimtazama Lissu.

Alisema familia yao inamuunga mkono Lissu katika harakati zake za kisiasa, akisisitiza kwa kauli: "Hata kama anatumia lugha ya ukakasi ambayo wengine hawapendi, labda inafika wakati ambao anasema liwalo na liwe, hatuwezi kuvumilia watu wengine watuchezee."

Katika hatua nyingine, michango ya fedha kwa ajili ya kumnunulia gari Lissu ulikuwa umefikia Sh. milioni 15.3 hadi jana mchana.

Lissu alithibitisha kufikia kiasi hicho cha fedha ndani ya siku mbili kupitia mtandao wake wa X na kuhamasisha wafuasi wake waendelee kumchangia ili lipatikane gari la kumsaidia katika harakati zake za kisiasa.

"Gari hili litawekwa kwenye Makumbusho kama mlivyoshauri. Gari mbadala linahitajika ili harakati za ukombozi ziendelee. Lengo ni kupata gari ndani ya mwezi mmoja. Ndani ya siku mbili, michango yenu imeshafikia Sh. 15,360,059. Kwa ukarimu wenu inawezekana," aliandika Lissu kwenye ukurasa wake huo.

Mwanaharaki Maria Sarungi anayeendesha harambee hiyo pia alithibitisha kufikiwa kiwango hicho cha fedha na kuhamasisha watu kuendelea kuchangia ili kufikia lengo ambalo halijatajwa, hata hivyo.

Katika shambulio hilo Lissu alirushiwa zaidi ya risasi 30. Kati yake, 16 zilimpata sehemu mbalimbali za mwili wake. Alipelekwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma kisha kuhamishiwa Hospitali ya Nairobi, Kenya na baadaye alipelekwa Ubelgiji kwa matibabu zaidi.


WE EFFECT

PREQUALIFICATION OF SUPPLIERS

REQUEST FOR PROPOSAL FOR GOODS AND SERVICES

We Effect invites application from reputable suppliers to be considered for inclusion in the Tanzania Country office list of prequalified suppliers for provision of goods and services for the year 2024.

**Deadline:** Friday 31ST May, 2024

Full details on the application process, see website

**https://weeffect.org/prequalification-of-suppliers/**


## Askofu azikwa kikanisa, ripoti polisi yasubiriwa

**Paul Mabeja na Peter Mkwavila,** DODOMA

KUKIWA na maswali mengi juu ya kifo cha Askofu Mkuu wa Makanisa ya Methodist Tanzania (MCT), Joseph Bundala (55), anayedaiwa kujinyonga, hatimaye mwili wake ulizikwa jana kwenye viwanja vya kanisa hilo Ihumwa, jijini Dodoma.

Wakati wa maziko ya mwili huo jana, uongozi wa kanisa hilo haukuweka bayana kilichosababisha uamuti kwa kiongozi wake huyo, ukisisitiza unasubiri ripoti za uchunguzi.

Askofu Bundala alikutwa amefariki dunia, akidaiwa kujinyonga ndani ya ofisi yake iliyoko kanisani huko, Mtaa wa Meriwa, Kata ya Ipagala, jijini hapo Mei 16, mwaka huu.

Akiongoza ibada ya kuuga mwili wa Askofu Bundala iliyofanyika nyumbani kwake Ihumwa, jijini Dodoma, Makamu Askofu Mkuu wa Kanisa hilo, Samweli Nyanza, alisema yote yaliyotokea na yanayosemwa wanamwachia Mungu.

"Wanasema sana kuhusu kanisa lakini kanisa litazidi kusimama imara, taarifa nyingi za vyombo vya habari zimeongezwa chumvi, maneno haya hata kwenye kanga yapo, sisi hatutaogopa maneno," alisema askofu huyo.

Alieleza kuwa baada ya tukio hilo kumekuwa na taarifa nyingi ambazo wanazipa tafsiri zina lengo la kudhoofisha kanisa.

Alisema kuwa wamefarijiwa na waraka wa Shekhe wa Mkoa wa Dodoma, Mustapha Rajab, aliyewataka kungalia mambo mawili; heshima ya kiongozi na heshima ya kanisa.

Askofu Nyanza alisema kanisa hilo ni miongoni mwa makanisa yenye misingi mizuri, akieleza kuwa Askofu Bundala alikuwa mcheshi na atakumbukwa katika maisha yake.

Akizungumza kwa niaba ya wamiliki wa shule binafsi Mkoa wa Dodoma, Mbunge wa zamani wa Dodoma, David Malole alisema umoja huo umepoteza mwanachama aliyekuwa na ushirikiano mzuri.

Diwani wa Ipagala, Dotto Gombo alisema watamkumbuka Askofu Bundala kutokana na kuwa mpenda maendeleo na aliyekuwa na ushirikiano mzuri na jamii.

Askofu Mkuu wa Elimu Pentekoste, Peter Konki, alisema wamepokea kwa masikitiko taarifa hiyo kwa kuwa Askofu Bundala alikuwa na ushirikiano mkubwa.

Akisoma wasifu wa marehemu, mwanafamilia Kikoti Lissu alisema Askofu Bundala alizaliwa Machi 18, 1969 kijiji Bubinza, wilayani Kishapu, mkoani Shinyanga akiwa mtoto wa sita kati ya 11 kwa Michae Bundala na mkewe Scolastika Pius.

Baada ya masomo ya sekondari alijiunga na jeshi na baadaye akajiunga na kanisa kutoa huduma za kiroho, akianzia uinjilisti, uchungaji na hatimaye askofu.

Alisema kuwa Askofu Bundala ameacha mke na watoto watatu, akisisitiza chanzo cha kifo chake kinachunguzwa.

Mwili wa Askofu Bundala uligundulika Meio 16 saa moja usiku ukiwa unaning'inia ofisini kwake.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Alchelaus Mutalemwa, alisema jeshi hilo linachunguza tukio hilo. Mwili uligundulika ndani ya ofisi yake iliyoko katika kanisa hilo.

Alisema kuwa uchunguzi katika eneo la tukio ulibaini kuwapo ujumbe unaoeleza kinachodaiwa sababu za kujinyonga ni madeni na mgogoro uliopo katika uendeshaji shule binafsi. Hata hivyo, kiwango cha fedha anachodaiwa hakijatajwa katika ujumbe huo.

## HABARI KITAIFA

# ACT yataka sheria kandamizi vyombo vya habari zifutwe

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimeitaka serikali kufuta sheria zote kandamizi na zinazopora uhuru wa vyombo vya habari na kutengeneza mpya kwa kushirikiana na wadau, zitakazolenga kuleta uhuru, weledi na ukuaji wa sekta ya habari nchini.

Aidha, kimeitaka serikali isimamie uanzishwaji wa Baraza Huru la Habari nchini ili kulinda na kutetea haki na maslahi ya wanahabari nchini.



Kauli hiyo ilitolewa jana na Waziri Kivuli wa Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Uchukuzi wa chama hicho, Rahma Mwita, wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, ikiwa ni uchambuzi wa bajeti ya wizara hiyo iliyosomwa bungeni juzi na waziri mwenye dhamana, Nape Nnauye.

"Katika miaka saba iliyopita, Tanzania imetunga sheria kandamizi zinazozuia uhuru wa vyombo vya habari, uhuru wa kujieleza na zinazokazia ukali wa sheria zilizopo ambazo ni vikwazo katika kuhabarisha wananchi," alisema Rahma.

"Sheria hizi ni pamoja na ile ya kupata habari ya mwaka 2016, kanuni za maudhui ya mtandaoni 2018, Sheria za makosa ya kimtandao 2015, Kanuni za jumla za 2016, na Sheria ya Takwimu 2015 pamoja na marekebisho yaliyofanywa kwa mujibu wa Sheria ya Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali Na. 3 mwaka 2018. Kwa pamoja, sheria hizi zinajinaisha uandishi wa habari za kina na za uchunguzi na zilikazia ukali wa sheria zilizopo ambazo ni vikwazo katika kuhabarisha wananchi."

"Tumeona Bunge la Jamhuri limepitisha mabadiliko ya Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016, Sura 229, lakini wadau wamelalamikia mambo kadhaa katika mchakato wa mabadiliko hayo kama vile mtindo uliotumika kuwasilisha mabadiliko hayo ambao ni mabadiliko ya sheria mbalimbali, jambo ambalo limefanya muswada huo kama jambo la jumla na si jambo mahususi linalohitaji mjadala mkubwa na maafikiano ya wadau."

Rahma alisema jambo jingine ni lugha iliyotumika na mchakato wa mabadiliko ulivyofichwa huku sehemu kubwa ya wadau wakishindwa kushiriki kwa sehemu kubwa kwenye mabadiliko hayo jambo ambalo bado yanaminya uhuru wa habari nchini.

Kuhusu deni la serikali kwenye vyombo vya habari, ACT-Wazalendo kiliitaka serikali kupitia bajeti kuu kuzingatia madai hayo na kutenga angalau asilimia 0.4 ya bajeti kwa ajili ya wizara ya habari, ili iweze kulipa madeni hayo kwa mkupuo.

**MAWASILIANO**

Kadhalika, chama hicho kiliitaka serikali kufanya marekebisho ya kanuni zinazosimamia vifurushi vya dakika za kupiga, mitandao ya intaneti na meseji ili kushusha gharama zake na kuongeza ushirikishwaji wa wananchi kuwezesha kudhibiti, uholela wa kampuni hizo kupandisha gharama hizo.

Kilisema katika hotuba ya bajeti ya serikali, waziri hakuzingatia wala kutoa hatua za kibajeti katika kushughulikia masuala hayo makubwa ya gharama za vifurushi na upatikanaji wa data na kwamba kuna haja ya serikali kuanzisha mchakato wa kutengeneza upya sera ya taifa ya mawasiliano.

Kilipendekeza ni vema mchakato huo ukawashirikisha watoa huduma, watumia huduma, wataalamu wa masuala ya kimtandao na wadau wengine.

Kuhusu kukatika nyaya za baharini, kiliitaka serikali kuwekeza kwenye njia mbadala ya satellite na kwenye utafiti wa anga ili kujitegemea kimtandao kwa ajili ya usalama wa taifa na kuitaka kuzisimamia kampuni za kutoa huduma za mitandao kutoa fidia kwa watumiaji kwa muda ambao shughuli zao zilisimama kutokana na tatizo la mtandao.

Pia kimetaka serikali itoe huduma ya data bure maeneo yote ya umma kama vile hospitali, shuleni, vyuoni, ofisini na maeneo ya masoko, kupunguza gharama za kodi katika miundombinu ili mtumiaji apate nafuu ya kupata huduma.

Rahma alisema serikali ina wajibu wa kuratibu na kusimamia huduma za mawasiliano ya simu na intaneti zikiwamo viwango vya uwekezaji, ubora na viwango wa huduma, gharama za huduma za uzalishaji na usambazaji.

Aidha, alisema katika mazingira ambayo sekta hii inakua kwa kasi bila kuratibu na kusimamia vizuri viwango vya huduma na gharama zake ni kuruhusu wananchi kunyonywa na kupitia mateso makubwa bila uangalizi.

Vile vile, kuna haja ya serikali kuanzia mwaka huu na miaka mitano ijayo kuwa na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) ambao unatengewa fedha za kutosha ili kuimarisha mtandao wa mawasiliano nchini.

**MATAPELI**

Kuhusu wimbi la utapeli mitandaoni, chama hicho kilisema kuna haja serikali ikashirikiana na wizara pamoja na taasisi nyingine kutambua biashara za mtandaoni kisheria ili kupunguza wimbi la utapeli.


## Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions ndio uende "pay via mobile". Itakuletea maelekezo namna ya kulipa kwa simu kulingana na mtandao unaotumia.
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia
6. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

7. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-6



Kwa mawasiliano zaidi Tupigie: 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Barua pepe: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

# Waziri aonya wanasiasa wanaoligeuza jeshi mtaji wao

**Na Jenifer Gilla**

WAZIRI wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Dk. Stergomena Tax, ameonya jeshi kuhusishwa na masuala ya kisiasa kwa kuwa limeundwa kwa ajili ya shughuli za ulinzi wa taifa.

Aliyasema hayo jana wakati akijibu hoja za wabunge na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama wakati wa mjadala wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka 2024/2025 aliyowasilisha bungeni.

Dk. Stergomena alisema migogoro inapojitokeza itatuliwe kwa mashauriano na kufuata sheria na taratibu zilizowekwa na si kisiasa.

Aidha, aliwataka wananchi na viongozi kuyalinda na kutoyavamia maeneo ya jeshi na kusababisha migogoro kwa kuwa yametengwa kwa ajili ya shughuli za ulinzi wa taifa.

Alisema kupitia Mpango wa Kutatua Migogoro ya Ardhi wa mwaka 2021/22 - 2023/24, wizara imeendelea kutatua migogoro hiyo na mpaka sasa 78 sawa asilimia 89.7 iliyotambuliwa imetatuliwa kwa njia ya mazungumzo na kuhuisha mipaka, kupima na kulipa fidia kwa wananchi wanaostahili.

Aliwatoa hofu wabunge kuwa hali ya mipaka ya nchi ni salama na wizara imeendelea kuliwezesha Jeshi la Ulinzi wa Wananchi wa Tanzania kwa zana na vifaa vya kisasa ili kuimarisha ulinzi.

Alisema wizara imewasilisha mapendekezo ya kurekebisha sheria ya kodi kwa Tume ya Kurekebisha Sheria ili vifaa vyote vinavyoingizwa nchini kwa matumizi ya jeshi visitozwe kodi.

Dk. Stergomena aliliomba Bunge liidhinishe bajeti ya Sh. trilioni 3.3 ili kutekeleza vipaumbele vyake ikiwamo kuendelea kuliimarisha jeshi kwa zana na vifaa vya kisasa, mafunzo na mazoezi, pamoja na rasilimali watu.

Alisema wizara hiyo pia imeweka kipaumbele katika kuendelea kuimarisha uwezo wa Jeshi la Kujenga Taifa kwa kuboresha miundombinu ili liweze kuchukua vijana wengi zaidi watakaopata mafunzo ya uzalendo, ukakamavu, umoja wa kitaifa na stadi za kazi kwa vijana wa kundi la lazima na wakujitolea.

Alisema pia wataimarisha ushirikiano na Umoja wa Mataifa (UN), Umoja wa Afrika (AU), jumuiya za kikanda na nchi mbalimbali katika nyanja za kijeshi na kiulinzi na kuimarisha diplomasia ya ulinzi na kuendelea kushirikiana na mamlaka za kiraia katika kukabiliana na majanga na dharura inapohitajika.

**MAONI YA WABUNGE**

Wameishauri serikali kuyaandaa na kuyawezesha ipasavyo majeshi ya ulinzi nchini ili yakabiliane na changamoto za karne ya 21 ikiwamo mbinu na medani za kivita zilizobadilika kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia.

Mbunge wa Kuteuliwa, Shamsi Vuai Nahodha, alisema katika karne hii vita vinapigana kwa kutumia teknolojia ya kisasa ikiwamo maroboti na mifumo ya 'cyber' hivyo taifa linawajibu wa kuangalia ni wapi jeshi limeachwa nyuma ili kuliimarisha.


Mbunge wa Viti Maalum, Neema Lugangira, aliishauri serikali iiongezee fedha wizara hiyo ili iwe na idara madhubuti ya kukabiliana changamoto zinazoweza kusababishwa na matumizi hasi ya kidijitali ambayo yameshamiri kutokana na maendeleo ya teknolojia.

Mbunge wa Jimbo la Nkasi Kusini, Vicent Mbogo, aliishauri jeshi hilo kuongeza ulinzi katika mipaka ya kwenye maziwa ikiwamo kujenga kambi za jeshi kwa kuwa jambo hilo limeleta usumbufu kwa wakazi wa maeneo hayo.

**USHAURI WA KAMATI**

Ilishauri serikali ifanye mapitio ya sheria za kodi zinazotoza vifaa vya jeshi ili kuweka utaratibu mzuri wa kutoa msamaha kwa vifaa vyote vinavyoingizwa kwa ajili ya matumizi ya jeshi.

Mwenyekiti wa kamati hilo, Vita Kawawa alisema kamati pia imeshauri wizara izibane taasisi za umma ili zilipe deni la Sh. bilioni 1.9 inazodaiwa na kampuni tanzu ya Shirika la Mzinga ili liweze kuendelea na majukumu yake ya ikiwamo uvumbuzi wa maboni ya kudhibiti wanyamapori waharibifu.



Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, akisalimiana na Mkurugenzi Mkuu wa Ecobank Tanzania, Charles Asiedu, alipowasili katika kikao kilichoangazia ushirikiano kati ya serikali na benki hiyo, jijini Dodoma. **PICHA: ECOBANK**

# Watumishi walioathirika uhakiki taarifa, vyeti wapandishwa vyeo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WATUMISHI 375,904 wamepandishwa vyeo wakiwamo 85,471 walioathirika na uhakiki wa taarifa za kiutumishi na vyeti vya elimu kwa watumishi wa umma kuanzia mwaka 2021/22 hadi sasa, serikali imesema.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwan Kikwete, aliyasema hayo jana bungeni alipojibu swali la Mbunge wa Iringa Mjini (CCM), Jesca Msambatavangu.

Mbunge huyo alihoji lini serikali itarekebisha madaraja ya watumishi wa umma, hasa walimu waliopandishwa na kunyang'anywa vyeo kuanzia mwaka 2016 hadi 2018 ili kupisha uhakiki wa wakati huo.

Akijibu swali hilo, Ridhiwani alisema kuwa mwaka 2016 serikali ilisitisha mambo mbalimbali ya kiutumishi ikiwamo upandishaji vyeo ili kupisha uhakiki wa taarifa za kiutumishi na vyeti vya elimu kwa watumishi wa umma.

"Katika kutatua changamoto zilizojitokeza kutokana na kusitishwa huko, mwaka 2021/22 serikali ilianza kutekeleza zoezi la kuwarejesha watumishi wa umma katika kada mbalimbali kwenye nafasi na vyeo vyao stahiki kwa njia mbalimbali ikiwamo msawazo wa vyeo na mserereko wa madaraja," alisema.

Ridhiwani alisema kuwa kwa mwaka 2023/24, serikali inatarajia kuwapandisha vyeo watumishi 81,503 wakiwamo walioathirika na zoezi la uhakiki wa taarifa na vyeti vya watumishi wa umma.

## Serikali yawatoa hofu wafanyabiashara ujenzi Soko la Afrika Mashariki

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, amewatoa hofu wafanyabiashara wa Soko la Kariakoo kuhusu Soko la Afrika Mashariki linalojengwa eneo la China Plaza, Ubungo, Dar es Salaam kuwa halitaua biashara zao.

Jana wakati wa semina ya wabunge iliyohusisha taasisi mbili zilizo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara ambazo ni Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Dk. Ashatu alisema tayari serikali imekaa vikao na wafanyabiashara hao mara tatu kujadiliana juu ya jambo hilo.

Alisema timu ya serikali iko kazini, inafanya kazi yake na katika mradi huo mpya, yanajengwa maduka 2,002 wakati Kariakoo kuna maduka 40,000.

Alisema wizara yake inashirikiana na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ambao ndio wenye Manispaa ya Ubungo kuona mkataba walioingia, umeingiwaje na wanakwenda nao vipi, pia wanashirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) kwa kuwa wao ndio wanaotoa vibali vya ufanyaji kazi nchini kwa wageni.

Alisema lengo ni kujua raia wa China wanaosemwa wanauza maua nchini, vibali vyao vinaonesha wamekuja kufanya nini nchini na timu hiyo itakapokamilisha kazi taarifa itapelekwa bungeni.

Pamoja na hayo, alisema zipo taarifa kuwa asilimia 98 ya watu waliomba kufanya biashara kwenye maduka hayo ni Watanzania na kuhoji "kama ndivyo Wachina watauaje Soko la Kariakoo?"

Alisisitiza wanaendelea kulifanyia kazi kwa umakini mkubwa na itakapofikia Julai mwaka huu wakati ambapo maduka hayo yatafunguliwa itajulikana ukweli kuhusu jambo hilo.

Mbunge wa Viti Maalum, Mwanaisha Ulenge, ndiye aliyeibua suala hilo, alipohoji juu ya jengo hilo, akisema kuwa badala ya Watanzania kwenda China, watapata mahitaji katika jengo hilo na kwamba hofu iliyoko mtaani ni kuwa wanakwenda kuua Soko la Kariakoo.

Akijibu hoja za wabunge zilizoibuliwa wakati wa semina hiyo, Mkurugenzi wa Idara ya Leseni BRELA, Andrew Mkapa alisema kuna haja kutoa elimu kwa Watanzania ili wajue haki zao wakati wanaingia ubia na wawekezaji wa nje ya nchi wakati wa kusajili kampuni na kwamba ni vigumu kujua kama Mtanzania atanyimwa haki yake anaposajili kampuni na wageni hao.

Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Dk. Athuman Ngenya alisema shirika hilo litaendelea kuboresha miundombinu na kuweka mazingira rafiki ya utoaji huduma kwa wakati ili kuchochea ufanyaji biashara na kuinua uchumi wa viwanda.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Brela, Godfrey Nyaisa alisema katika kipindi cha miaka saba kupitia mfumo wa usajili kielektroniki (ORS), kuna ongezeko la kampuni zilizosajiliwa kutoka 119,000 hadi kufikia 205,000 Mei mwaka huu.

Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, Dk. Medard Kalemani, alipongeza serikali kwa kuzifanyia mageuzi makubwa TBS na BRELA ambazo zilikuwa na changamoto kubwa ya kiutendaji.

HABARI KITAIFA

# Sababu vijana kutopiga kura

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Viti Maalum, Nusrat Hanje amesema tatizo la kiuchumi kwa vijana ni kikwazo kwa kundi hilo kushiriki kwenye uchaguzi.

Aliyasema hayo jana jijini Dodoma alipozungumzia mdahalo wa vijana utakaofanyika Mei 25, 2024 unaolenga kuzungumzia miaka mitatu ya Rais Samia Suluhu Hassan, Hanje.

Alisema kuwa pamoja na mambo mengine, mkutano huo utakwenda kuweka viwango vya aina ya vijana wanaohitajika Tanzania.

Mbunge huyo alisema kuwa katika mdahalo huo watajadili ushiriki wa vijana kuwania nafasi mbalimbali za uongozi.

Alisema ni vyema vijana wakawania nafasi kuanzia katika serikali za mitaa na vijiji hadi ngazi za kitaifa. Vyama vya siasa vina jukumu la kuweka vijana chini ya miaka 35 kwenye uteuzi wa wagombea.

"Lakini kuna changamoto za kiuchumi kwa vijana chini ya miaka 35, hasa katika wabunge wanaume. Wao hawana nafasi ya viti maalum, ni lazima ukagombee, kijana gani anaweza kuwa na uwezo wa kiuchumi kwenda kuchangia?" Alisema.

Nusrat alisema hata kuendesha kampeni kunahitaji fedha, lakini kijana ndio kwanza ametoka chuoni, "anajitafuta kiuchumi" ili kupata fedha za vipaza sauti na magari ya kufanya kampeni.

Alisema taifa linahitaji vijana ambao wanaweza kujenga hoja, wanaoweza kushauri, siyo kusifia tu viongozi. Hata Rais Samia Suluhu Hassan alishasema "serikali ikosolewe kwa hoja.

Mbunge huyo alisema ni matumaini yake kuwa baada ya mkutano huo watakuwa na vijana wanaoweza kujenga taifa na si wabeba mikoba ya viongozi au "chawa" ambao hawashauri panapohitajika.

"Isionekane kama ni 'uchawa' mtu akiamua kuzungumzia vizuri kiongozi wake kama amefanya vitu vizuri. Mahali ambapo unatakiwa kushauri bado unasifia, wakati mwingine labda mwenyewe amekwama anatakiwa kushauriwa, lakini wewe unasifia. Tutajadili hilo," alisema.

Mbunge huyo alisema mdahalo huo utahusisha makundi ya vijana kutoka jumuiya ya vyama vya siasa, asasi za kiraia, viongozi wa dini na wanafunzi kutoka taasisi mbalimbali za elimu.

Alisema wawakilishi wa wizara zinazojishughulisha na masuala ya vijana watashiriki pia katika mdahalo huo pamoja na viongozi wa vijana kwenye vyama vya siasa vya CCM, ACT-Wazalendo, CUF na vingine.

# Wanafunzi 480 waketi sakafuni

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

ZAIDI ya wanafunzi 480 katika Shule ya Msingi Kimpungua, Manispaa ya Singida wanalazimika kusoma wakiwa wameketi sakafuni kutokana na ukosefu wa madawati.

Hayo yalibainishwa juzi wakati wa kikao cha wananchi kilichoitishwa na Kamati ya Shule ya Msingi Kimpungua kwa ajili ya kujadili changamoto zinazokabili shule hiyo na kuangalia namna ya kuzipatia ufumbuzi.

Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Hedwiga Mtalo, aliwaeleza wazazi na wajumbe hao kuwa shule hiyo yenye jumla ya wanafunzi 1,182 inakabiliwa na upungufu wa madawati 162 ambao unasababisha wanafunzi 486 kusoma wakiwa wameketi sakafuni.

Alisema tatizo hilo ambalo ni la muda mrefu limetokana na ongezeko kubwa la wanafunzi, akifafanua kuwa mwaka 2013 wakati shule inaanzishwa ilikuwa na wanafunzi 63 tu.

Alsiema changamoto ya upungufu wa madawati ingekuwa ilishapatiwa ufumbuzi kama wananchi wangekuwa wanatekeleza makubaliano wanayopeana kwenye vikao jinsi ya kumaliza tatizo hilo. Ibara ya 8 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977, inaelekeza wananchi kushiriki katika shughuli za serikali yao.

"Watoto wanakaa chini na kuna darasa moja halina madawati kabisa na madarasa mengine, dawati moja wanakaa wanafunzi wanne, hali inayosababisha madawati kuvunjika na changamoto hii tungekuwa tulishaimaliza kama wazazi wangekuwa wanatekeleza tunayokubaliana kwenye vikao," alisema.

Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 iliyofanyiwa marejeo mwaka jana, inaelekeza shule za msingi ziwe na madawati na yatumike kwa uwiano wa 3:1; yaani wanafunzi watatu kwa dawati moja.

Diwani wa Misuna, Hamis Kisuke alisema hali katika shule hiyo inatisha. Peke yake hawezi kumaliza changamoto iliyopo katika shule hiyo, hivyo kinachohitajika ni ushirikiano wa wananchi.

"Serikali imetupa madarasa, sisi kama wazazi jukumu letu ni kuweka madawati ili watoto wetu wasome vizuri na wao waje wazae vizuri kama ninyi mlivyowazaa. Hili ni jambo endelevu na si la wiki moja tu," alisema.

Mwenyekiti wa Kamati ya Shule hiyo, Ibrahimu Yohana, alitoa ombi kwa serikali kuingilia kati kusaidia kutatua changamoto hiyo ya ukosefu wa madawati kwenye shule hiyo.

"Kama inavyosemwa na wahenga, 'uchungu mwana aujua mzazi'. Serikali ni kama mama yetu, inatupa madarasa na inapaswa pia kutupa na madawati kwa sababu ukinijengea nyumba halafu hujanipa kitanda, unakuwa hujanisaidia sana," alisema.

Ofisa Elimu Msingi Manispaa ya Singida, Omari Maje, alisema wananchi wamekubaliana katika mkutano kuchangishana kila mmoja Sh. 6,000 kwa ajili ya kununua madawati 81 ya kuanzia ili kuunga mkono jitihada zinazofanywa na serikali katika kuboresha elimu.

Alisema kuwa kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024, serikali imetoa Sh. milioni 40 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa mawili katika shule hiyo, mradi ukihusisha pia ununuzi wa madawati 32.

Kimsingi, kinachoshuhudiwa katika shule hiyo ni ishara ya kutotekelezwa kwa hoja ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka 2017.

Machi 2017, CAG (kipindi hicho, Prof. Mussa Assad) alitoa Ripoti ya Ukaguzi Maalum wa Miundombinu na Samani za Shule za Msingi nchini, akibaini uhaba mkubwa, hali kadhalika uchakavu wa miundombinu na samani za shule za msingi zinazomilikiwa na serikali.

Akatoa hoja kwamba serikali ijenge miundombinu mipya kukabiliana na kasi ya ongezeko la wanafunzi ambayo ni ya asilimia tano kwa mwaka, pia kukarabati miundombinu iliyochakaa.



Kazi ya kusafisha eneo kwa ajili ya kuanza ujenzi wa njia ya mabasi ya mwendokasi ikiendelea katika barabara ya Sam Nujoma, Dar as Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Utaratibu ajira wahitimu la VII waondolewa JWTZ

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

UTARATIBU wa kuandikisha ajira kwa vijana wanaohitimu elimu ya darasa la saba kwenye Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) umeondolewa, serikali imeliarifu Bunge.

Naibu wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, aliyasema hayo jana bungeni alipojibu swali la Mbunge wa Ushetu (CCM), Emmanuel Cherehani.

Mbunge huyo alitaka kauli ya serikali juu ya mpango wa kuongeza nafasi za ajira na mafunzo jeshini kwa vijana wanaohitimu darasa la saba na kidato cha nne.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Pinda alisema JWTZ huandikisha askari wapya kwa mujibu wa sheria, kanuni na maelekezo yanayotolewa mara kwa mara.

"Utaratibu wa kuandikisha jeshini askari wapya umefanyiwa kwenye Kanuni ya 5 ya Kanuni za Majeshi ya Ulinzi Juzuu ya Kwanza (Utawala). Serikali imeondoa utaratibu wa kuandikisha ajira kwa vijana wanaohitimu elimu ya darasa la saba," alisema.

Kuhusu kuongeza idadi ya ajira na mafunzo jeshini kwa vijana wanaohitimu kidato cha nne, Naibu Waziri Pinda alisema hutegemea bajeti inayotengwa kwa mwaka husika.

"Jeshi huandikisha askari wapya baada ya kupewa maelekezo na idadi ya nafasi kulingana na uwezo wa kibajeti, nafasi hizi hugawanywa kulingana na mahitaji ya kitaaluma na ujuzi," alisema.

Akiuliza swali ya nyongeza, Mbunge Cherehani alisema hakuna uwiano wa vijana wanaoingia katika mafunzo na wale wanaoajiriwa na kuhoji mkakati wa muda mfupi na muda mrefu wa serikali kuhakikisha vijana wanaajiriwa.

Pia alisema vijana hao wanapokuwa katika mafunzo kumekuwa na changamoto ya miundombinu na kuhoji mkakati wa serikali kukabiliana na tatizo la miundombinu.

Naibu Waziri Pinda, akijibu maswali hayo, alisema suala la ajira linategemea nafasi zinazotolewa na serikali.

Kuhusu miundombinu, Pinda alisema serikali imekuwa ikiviangalia vyombo vya ulinzi na usalama kwa upekee na hivyo hakuna uhakika wa ukosefu wa vifaa na miundombinu ya mafunzo katika kambi za jeshi.

Alisema serikali imeweka miundombinu wezeshi kwa vijana ili kupata mafunzo wezeshi yatakayowasaidia kumaliza mafunzo yao.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Utaratibu madaktari bingwa kuweka kambi unasaidia

**KUMEKUWA** na utaratibu wa kusaidia wananchi wanaosumbuliwa na magonjwa mbalimbali kwa madaktari bingwa kuweka kambi na kuwapima afya zao ili kubaini tatizo na kupatiwa ushauri wa tiba.

Utaratibu huu unasaidia hasa kwa watu wasiokuwa na uwezo wa kwenda hospitalini kila mara kupima afya zao na kujua magonjwa yanayowasumbua.

Kupitia utaratibu huo, wagonjwa zaidi ya 3,000 kutoka katika wilaya za Mkoa wa Morogoro wamenufaika kwa kupatiwa huduma za tiba na upasuaji kutoka kwa madaktari bingwa wa Dk. Samia Suluhu Hassan, walioweka kambi kwenye hospitali ya rufani ya mkoa huo.

Madaktari bingwa hao wamepangiwa kutoa huduma katika kambi ya Kanda ya Kati inayojumuisha mikoa ya Morogoro, Pwani, Iringa na Singida.

Kwa mujibu wa maelezo kutoka katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro, Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Mifupa kutoka Hospitali ya Tumbi, Kibaha mkoani Pwani, Dk. Amani Malima, mafanikio hayo yametokana na idadi kubwa ya wagonjwa kujitokeza kupata huduma hizo.

Dk. Malima ambaye ni Mwenyekiti wa Kambi ya Kanda hiyo iliyokuwa na madaktari bingwa na bingwa bobezi zaidi ya 50, awali katika programu hiyo ilikuwa ni kuwaona wagonjwa 2,000, lakini hadi kufikia tamati ya siku tano zilizowekwa wagonjwa 3,128 walionwa.

Kwa mujibu wa madaktari hao bingwa lengo la awali la wagonjwa watakaofikiwa, walikadiria kufanya upasuaji kwa watu 100, lakini kutokana na mwitiko mkubwa wagonjwa 109 walifanyiwa upasuaji na wote walitoka salama, wakati wagonjwa 37 walipatiwa rufani kwenda hospitali za kikanda na kitaifa.

Huduma hii imesaidia kuokoa afya za wananchi waliokuwa na tatizo, lakini kutokana na kutokuwa na uwezo wa kulipia gharama walibaki nyumbani wakiteseka na ugonjwa.

Kutoka katika kambi hiyo imegundulika kuwa magonjwa yaliyoongoza ni yasiyoambukiza ama magonjwa ya ndani yakiwamo ya shinikizo la juu la damu, kisukari na moyo.

Na kwa upande wa Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Ndani, Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro, idara yake ya magonjwa ya ndani ilikuwa na wagonjwa wengi akitoa mfano wa siku mbili za mwanzo ilipokea wagonjwa 649.

Rais Samia Suluhu Hassan, amefanya jambo kubwa la kuwasaidia wananchi hao ambao wamefurahi na huduma zilizotolewa na walitamani ziwe endelevu.


Baadhi ya wanufaika na huduma iliyotolewa na madaktari bingwa hao wameshukuru kwa huduma hiyo kutolewa mkoani mwao na kuwezesha wagonjwa wengi kufanyiwa uchunguzi na kupatiwa matibabu kwa gharama nafuu.

Madaktari hao wamewasaidia wananchi wengi ambao hawakuwa na uwezo na kwa mujibu wa wananchi hao wamemwomba Rais na wabunge waendelee kuwaletea huduma hizo ili wananchi wanufaike kwa kuwa maradhi ni mengi na wagonjwa ni wengi.

Hata hivyo, imependekezwa kuwa muda wa kuwekwa kambi uongezwe ili wananchi wengi waweze kufaidika na huduma hiyo kutokana na mwitikio wa watu waliojitokeza kuwa mkubwa.

Pia Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima, amemshukuru Rais Dk. Samia kwa kuwaleta madaktari bingwa mkoani humo na kuleta faraja kwa wananchi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# Marufuku ya wizara bweni isimamiwe

**ELIMU** imepewa kaulimbiu nyingi, ikiwamo ya elimu 'ni ufunguo wa maisha,' 'haina mwisho' yote hayo ni kutokana na umuhimu katika maisha. Hivyo, wazazi na walezi wamekua wakijitahidi ili watoto wapate elimu bora.

Kwa sasa wapo baadhi ya wazazi na walezi ambao hupeleka watoto wenye umri wa kusoma shule za awali au darasa kwanza hadi la nne katika shule za bweni, lengo likiwa ni kusaka elimu bora.

Pamoja na hayo, nadhani ipo haja ya kuangalia baadhi ya vitu ili kuwaepusha watoto hao na madhara yanayotokana na kuishi bweni badala ya kutunzwa ndani ya familia zao.

Ninaeleza kwa sababu wataalamu wa saikolojia wanasema mtoto mdogo ubongo wake ni kama karatasi nyeupe ambayo haijaandikwa chochote, na kwamba kadri anavyopata ufahamu ndivyo anavyoyaingiza vitu kichwani mwake.

Kwa maelezo yao ni, mtoto wa umri mdogo wa kuanzia miaka ziro hadi mitano anapaswa kuishi na wazazi badala ya kupelekwa bweni ambako hawezi kulelewa kama ambavyo angelelewa kwao.

Aidha, wanasema kuna madhara ya muda mrefu yanayotokana na mtindo wa kuweka watoto hao bweni, ikiwamo kukosa mapenzi kwa wazazi na jamii yao na kushindwa kuwa sehemu ya familia pia.

**Kwa sasa wapo baadhi ya wazazi na walezi ambao hupeleka watoto wenye umri wa kusoma shule za awali au darasa kwanza hadi la nne katika shule za bweni, lengo likiwa ni kusaka elimu bora.**

Zipo sababu mbalimbali zinazochangia baadhi ya wazazi na walezi kupeleka watoto wao shule za bweni, ikiwamo kufiwa na wenzao wao, majukumu ya kila siku na pia kutafuta elimu bora.

Lakini suala la makuzi bora ni lazima lizingatiwe ili kuepuka mmomonyoko wa maadili ambao umekuwa ukijitokeza kwa baadhi ya vijana ambao huenda walilelewa katika mazingira hayo ya bweni.

Hata Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeshaelekeza kuwa hairuhusiwi kutolewa huduma ya bweni kwa wanafunzi wa elimu ya awali na darasa la kwanza hadi la nne.

Wizara inaeleza kuwa kama italazimika kutolewa kwa huduma hiyo, basi iwe ni kwa kibali maalum ambacho kimetolewa na Kamishna wa Elimu baada ya kupokea maombi rasmi kutoka kwa mdau husika.

Kwa mujibu wa wizara baadhi ya shule zimekuwa zikipokea watoto wenye umri mdogo kuanzia darasa la awali hadi la nne, huku huduma zinazotolewa kwa wanafunzi hao zikiwanyima fursa ya kuungana na familia na jamii zao, kujenga maadili na kushiriki katika shughuli mbalimbali za maendeleo ya familia zao.

Ninaungana na serikali kwa uamuzi huo, kwani unalenga kuimarisha malezi yanayotolewa na wazazi na walezi kwa mtoto badala ya kuwaachia watumishi wa shule.

Walimu ni wazazi wa pili kwa mwanafunzi, lakini kwenye suala la wanafunzi wenye umri mdogo kuishi bweni, huko wanasimamiwa na watu wengine ambao wanawasimamia.

Sina maana kwamba hawafai, bali ni suala la umri wa wanafunzi, kwamba kwa udogo wao wanatakiwa kuwa chini ya usimamizi wa wazazi ili wajue tabia zao na kuwarekebisha ili waende sawa.

Vilevile, sidhani kama msimamizi wa bweni anaweza kuwalea watoto wote vizuri. Lakini kwa mtindo huo wa kuweka bweni, mapenzi ya watoto yanaweza kuwa wasimamizi hao badala ya wazazi.

Hivyo, kama hakuna sababu zozote za msingi za kumpeleka mdogo bweni, ni vyema akasoma shule za kutwa na kurudi nyumbani ili wazazi na walezi waweze kukaa naye na kumfundisha maadili mema.

Iwapo itamlazimu mzazi kupeleka mtoto bweni, basi ni vyema awe anafualitia maendeleo yake mara kwa mara na kujua marafiki wa mtoto badala ya kumwacha tu, kwani mtindo huo unaweza kusababisha asiwe karibu na mzazi na kuelekeza mapenzi wale walio karibu naye.

HABARI KITAIFA

## 'Tunduru ipewe hadhi ya mkoa'

**Na Stevie chindiye,** TUNDURU

SERIKALI imeombwa kuangalia uwezekano wa kuipatia hadhi ya kuwa mkoa Wilaya ya Tunduru ili kusogeza huduma kwa jamii.

Mwakilishi wa Shekhe wa Wilaya ya Tunduru, Shekhe Abdalah Kawanga, alitoa hoja hiyo mwishoni mwa wiki wakati akisoma dua kwenye Mkutano Mkuu wa Chama Kikuu cha Ushirika Tunduru (TAMCU) wilayani hapa.

Shekhe Kawanga alisema kuwa Tunduru ni miongoni mwa wilaya kongwe nchini na ina eneo kubwa kiutawala kulinganishwa na maeneo mengine ya utawala.

Hata hivyo, maombi ya kuipa hadhi ya mkoa wilaya hiyo yamekuwapo kwa muda mrefu, viongozi mbalimbali wakifanya hivyo. Tayari taratibu za maombi ya kugawa wilaya kuwa na halmashauri mbili, majimbo, wilaya mbili na taratibu nyingine za kisheria zimetekelezwa. Kinachosubiriwa ni tamko la serikali.

Shekhe Kawanga pia akatumia nafasi hiyo kukumbusha serikali kutekeleza ahadi yake ya kuijenga kwa kiwango cha lami barabara ya Tunduru-Nalasi-Mtwara.

Alisema barabara hiyo ni ukombozi kwa wananchi wa ukanda huo wa eneo la mpaka wa nchi za kusini mwa Afrika kupitia nchi jirani ya Msumbiji.

Alisema kujengwa barabara hiyo kwa kiwango cha lami ni ahadi ya Rais wa Rais Samia Suluhu Hassan. Alipofika wilayani Tunduru wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu wa 2020 (wakati huo akiwa mgombea mwenza Dk. John Magufuli).

Shekhe Kawanga pia aliwataka viongozi waliochaguliwa kwenye vyama vya msingi vya wakulima na watakaochaguliwa katika Uchaguzi Mkuu wa TAMKA, kufanya kazi kwa weledi ili kuwaletea maendeleo wakulima wa Tunduru.

Alisema tabia za baadhi ya viongozi wasio waadilifu kuwaibia wakulima zinasababisha manung'uniko yanayokatisha tamaa kundi hilo (wakulima).

Wilaya ya Tunduru ilianzishwa mwaka 1905 kipindi cha utawala wa ukoloni ambapo Serikali ya Ujerumani ilijenga boma katika eneo la Kadewele karibu na lilipo jengo la Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa sasa.

Ni miongoni mwa wilaya sita za Mkoa wa Ruvuma. Upande wa kaskazini inapakana na Mkoa wa Lindi, Mkoa wa Mtwara kwa upande wa mashariki, Namtumbo upande wa magharibi na nchi ya Msumbiji kwa upande wa kusini.

Kwa mujibu wa matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi iliyofanyika Agosti 2022, wilaya hiyo ina wakazi 412,054. Kati yao, wanaume ni 201,668 na wanawake ni 210,386.

Idadi kubwa kubwa ya wakazi wa Tunduru ni Wayao ambao wamehamia toka nchi jirani ya Msumbiji. Makabila mengine yanayopatikana wilayani Tunduru ni pamoja na Wamakua, Wangoni, Wanindi, Wandendeule, Wamatengo na Wasukuma.

Wilaya ya Tunduru ina jumla ya tarafa saba na kata 39. Tarafa hizo ni Namsakata, Nampungu, Nalasi, Matemanga, Nakapanya, Lukumbule na Mlingoti.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan katika Mkutano wa Dharura wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika SADC. Ameshiriki mkutano huo kwa njia ya mtandao katika ukumbi wa Waziri Mkuu, Mlimwa jijini Dodoma, jana. Anayezungumza naye ni Mwenyekiti wa Mkutano huo ambaye ni Rais wa Angola, Joao Lourenco. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Mbaroni kwa tuhuma kuuza dawa bandia za binadamu

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MAMLAKA ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi wanamshikilia Chacha Ngasa, mkazi wa Mtaa wa Kata ya Zongomela, wilayani Kahama, mkoani Shinyanga kwa tuhuma za kufanya biashara ya dawa bandia za binadamu zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni tano.

Vilevile, wamebaini kuwapo duka lenye dawa hizo lililofunguliwa kwa jina la Shalom Med Smart katika Mtaa wa Mwime. Ni baada ya wananchi kulalamika kutumia dawa zake bila kupona maradhi yanayowasumbua.

Mkaguzi wa Dawa kutoka TMDA, Venancy Burushi, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki alipozungumza na Nipashe muda mfupi baada ya kukamatwa kwa mmiliki wa duka hilo na kudai kuwa mtuhumiwa ametenda kinyume cha Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba, Sura 219.

Alitaja dawa zilizokamatwa kuwa ni pamoja na Tinidazole, Good Morning na Cafenol. Alidai kuwa zote zilikuwa zimekwisha muda wake wa matumizi lakini mmiliki wa duka aliendelea kuziuza kwa wananchi huku akijua wazi ni kosa kisheria na akibainika adhabu yake ni kubwa.

"Dawa zote hizi tulizokamata zimeghushiwa muda wa matumizi ambapo zipo zinaoonesha zimekwisha matumizi Desemba mwaka 2023 na zingine zimeongezwa muda wa matumizi, unaisha Septemba 24, mwaka huu lakini zimeongezwa muda hadi Oktoba 2025," alisema Burushi.

Meneja wa TMDA Kanda ya Ziwa Magharibi, Dk. Edgar Mahundi alisema dawa zote zilizokamatwa zimethaminishwa na gharama yake ni Sh. milioni tano. Kama zingeuzwa kwa binadamu zingeleta madhara makubwa ikiwa ni pamoja na kupata tatizo la usugu wa dawa mwilini.

Alisema mtuhumiwa atafunguliwa mashtaka kwa kukiuka sheria za uuzaji dawa za binadamu. Aliwataka wafanyabiashara wa dawa za binadamu kuacha tabia ya udanganyifu kwa kucheza na maisha ya binadamu.

Mkazi wa Mtaa wa Mwime, Hassan Said, alidai kuwa wiki mbili zilizopita ndugu yake alipata madhara kiafya baada ya kupewa dawa kutibu maradhi yaliyokuwa yanamsumbua.

Alidai walipokwenda kwa mmiliki wa duka hilo kumwuliza "kulikoni?" alikuwa mkali na kuwafukuza. Ni jambo analolitaja liliwasukuma kutoa taarifa kwa mwenyekiti wa mtaa na kuomba serikali imwajibishe.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Mwime, Dogo Mhenziwa, alikiri ofisi yake kupokea malalamiko juu ya wananchi kuuziwa dawa bandia na wamekuwa wanatoa taarifa lakini hakuna hatua zilizokuwa zinachukuliwa.

Alidai kuwa mmiliki wa duka hilo amekuwa akikamatwa na polisi mara kwa mara kwa tuhuma za kuuza dawa bandia lakini amekuwa akiachiwa na kuendelea kuuza dawa. Alisema anaamini kufungwa kwa duka hilo kutasaidia kudhibiti udanganyifu katika biashara ya dawa.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
20.05.2024

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe **24.05.2024 hadi 30.05.2024** kampuni ya **CEVA Interfreight** itasafirisha magari matupu wenye vipimo vikubwa kutoka **Mzenga** kuelekea **Bandari ya Dar Es Salaam,** gari hilo lenye namba za usajili **NRB97300 / NRB54202 DS00TG GP / NRB53910**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **Mita** | **36.5** |
| **Upana** | - | **Mita** | **4.30** |
| **Kimo** | - | **Mita** | **4.60** |

3. Njia itakayotumika: **Mzenga hadi Bandari ya Dar Es Salaam** kupitia **Barabara ya Morogoro, Barabara ya Mandela** gari litasafiri muda wa mchana ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni).***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***



Balozi wa China nchini, Chen Mingjian (wa pili kulia), akikabidhi gitaa kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji ambaye ni Mbunge wa Ubungo, Prof. Kitila Mkumbo, wakati wa hafla ya kukabidhi vifaa vya muziki na michezo kwa Shule ya Msingi Mlimani, Dar es Salaam jana. Kulia ni Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Florence Karara. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

SAKATA MTOTO KUBAKWA

# Polisi kutumia intelijensia

**Na Romana Mallya**

SIKU mbili baada ya gazeti hili kuripoti tukio la kubakwa na kunyongwa binti wa miaka 10 kijijini Mipera, Kata ya Marui, wilayani Kisarawe, mkoani Pwani, huku zikipita siku tisa bila mtuhumiwa kukamatwa, Jeshi la Polisi limetuma intelijensia yake na kuwapa mashekhe jukumu zito.

Juzi, Nipashe iliripoti tukio la mtoto (jina linahifadhiwa) mwanafunzi wa darasa la tatu, kufanyiwa ukatili huo na mtuhumiwa Ismail Mandanga, Kijiji cha Mianzi, ambaye sasa anawatishia wananchi na viongozi wa kijiji kwa panga.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Pius Lutumo, ambaye alipata taarifa za tukio hilo juzi kutoka kwa mwandishi wa habari hizi na kuahidi kufuatilia, alipotafutwa jana, alisema tayari ameshatuma intelijinsia yake.

"Baada ya taarifa nilifuatilia kwa OCD (Mkuu wa Polisi Wilaya) Kisarawe. Ni kweli tukio lipo limetokea siku za nyuma, lakini katika makosa kama haya huwa tunaangalia kosa kubwa na hapa ni la mauaji. Nimemwambia OCD asimamie mtuhumiwa akamatwe. Nategemea atakamatwa.

Kuhusu mtuhumiwa kutishia wananchi, Kamanda alisema alipoongea na OCD alithibitisha mtuhumiwa huyo kuonekana kwa kificho.

"Anaonekana kwa kificho, lakini tumetuma intelejensia katika maeneo hayo ndiyo maana nimesema tunategemea siku za karibuni tutamkamata," alisema.

Alisema kwa sasa polisi wamesambazwa kwenye kata ambako kuna wakaguzi ambao moja ya maelekezo ni kufanya mikutano ya hadhara, kuongea na wananchi kuacha matendo hayo, wasihofu kutoa ushahidi au kutoa taarifa yoyote.

**MAAGIZO MASHEHE**

Shekhe wa Wilaya ya Kisarawe na Mwenyekiti Mwenza Kamati ya Amani na Mjumbe Kamati ya Maadili ya Mahakama, Ramadhan Kumbangulu, amesema pamoja na kulaani kitendo hicho ambacho hata vitabu vya dini vinakemea na kupinga, tayari wameshatoa maelekezo kwa mashehe.

"Uislamu unakataza mambo haya. Si jambo zuri. Nilipopata taarifa nilimpigia OCD Kisarawe kumweleza na viongozi wa dini hili jambo tumesema hatuwezi kukubali, tutalifuatilia mpaka mtuhumiwa akamatwe.

**HALI ILIVYO**

Shehe Kumbangulu amesema jiografia ya Kisarawe ni tofauti na sehemu nyingine, imekuwa ni ngumu kijiografia, mazingira ya kiuchumi ni duni na wakati mwingine matukio kama hayo yanapotokea inakuwa vigumu kusaidia, kutokana na watu wake kukosa elimu na woga.

Shekhe Kumbangulu anasema juhudi kubwa zinazofanyika ni kufanya makongamano na kutembelea kata kuelimisha jamii.

**SMAJATA WAFUNGUKA**

Suala la elimu limeungwa mkono pia na Mwenyekiti wa Kampeni Huru ya Kitaifa ya Kupinga Ukatili (SMAUJATA), Shujaa wa Maendeleo na Ustawi wa Jamii Tanzania, Wilaya ya Kisarawe, Anectus Asingizibwe, akisema matukio hayo yamekuwa yakijitokeza wilayani humo na changamoto ikiwa ni uelewa mdogo wa watu namna ya kuripoti au kuzuia.

"Mtu anabakwa anakuja kutoa taarifa baada ya siku tatu, hata taratibu za kitabibu zikifanyika haziwezi kuona kitu. Mtu anabakwa, analawitiwa unamwogesha, ukija kumfikisha hospitalini kama ameoga huwezi kuona chochote.

"Mwisho wa siku watasema amebakwa, lakini ushahidi hakuna. Wananchi wanaishi maisha ya ujamaa sana na matukio haya yanapotokea mengi hufichwa."

Asingizibwe anasema SMAUJATA ina miaka mitatu wilayani humo tangu mwaka 2022 wakielimisha wananchi na kueleza kuwa, Kiluvya imekuwa na matukio mengi ya ubakaji ambao unakosa ushahidi baada ya kupotea.

Amesema udhibiti wa matukio hayo ni mgumu kwa kuwa wananchi huogopa kutokana na ujirani mwema au kuhofia kuvunja undugu na huamua hukaa kimya.

"Kwa hiyo Wilaya ya Kisarawe na Pwani kwa ujumla imekuwa ikikatiliwa kwa namna hiyo. Kwa ujumla matukio mengi tunayafikisha mbele, lakini yanakosa ushahidi."

**JUHUDI ZINAZOFANYIKA**

Ni kuhakikisha wanapata vibali vya halmashauri kwenda kwenye shule zote za msingi na sekondari.

Wamekutana na wanafunzi wa shule mbalimbali kuwaelimisha masuala ya ukatili, kufungua vilabu vya kupinga ukatili shuleni na kukutana na vyama vya walimu wilayani humo kupitia mikutano yao ya mwaka ya vyama vya walimu.

Kadhalika, amefanya mikutano na viongozi wa dini wilayani humo wanaoitwa Kamati ya Amani ya wilaya, ambayo Mwenyekiti wake ni Shekhe Mkuu wa wilaya na kushirikiana nao kufikisha elimu ya huduma ya msaada.

**MWANANCHI JASIRI**

Mariamu Kombe, Mwenyeji wa Marui Mwisho, anathibitisha kuwapo kwa uoga wa wananchi kutoa taarifa za matukio ya ukatili ingawa anasema, aina ya tukio hilo lilimfanya kujitoa kimasomaso.

"Nilipokea taarifa za tukio kutoka kwa mwanachi wa kijiji kulikofanyika unyama huu. Lakini nikaambiwa hawaoni juhudi za viongozi kumsaka mtuhumiwa.

"Nikatafuta namba katika simu yangu, nikakuta namba nimeandika kiongozi wala simjui nikampigia kumjulisha, akaniomba namba za viongozi wa kijiji, nikatafuta nikampa akaahidi kulifuatilia," anasema.

Mtoto huyo alifanywa ukatili huo baada ya mtuhumiwa kwenda nyumbani kwao anakoishi na babu na bibi na kumlaghai ampeleke shambani aliko babu, ndipo akampeleka porini na kumfanyia hivyo.

# JKT Ruvu wajizatiti kwa utalii

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

KIKOSI cha Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) Ruvu kinatarajia kuongeza wanyama, wakiwamo simba katika bustani yake iliyoko Ruvu, wilayani Kibaha, mkoani Pwani.

Bustani hiyo ya wanyama iko katika eneo la ekari 70 zilizotengwa na kikosi hicho kwa lengo la kuwarahisishia wananchi kuona wanyama wa aina mbalimbali na kupiga picha.

Kamanda wa Kikosi cha JKT Ruvu, Kanali Peter Mnyani, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki wakati wa uzinduzi wa bustani hiyo, akisema kuwa kwa sasa imeanza na wanyama wachache, wakiwamo pundamilia, swala, mbuni na twiga katika awamu ya kwanza.

Kanali Mnyani alisema mwezi Juni mwaka huu, awamu ya pili ya wanyama watakaopelekwa katika bustani hiyo ni pamoja na simba na kabla ya kuwekwa kwenye bustani hiyo watapatiwa mafunzo ambayo yatamwezesha mtu yeyote kupiga nao picha bila kumdhuru.

Kamanda huyo alisema kuanzishwa bustani hiyo kutasaidia kukuza uchumi kwa kuongeza pato litakalosaidia kuhudumia vijana wanapofika kupata mafunzo katika kikosi hicho.

Akifungua bustani hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, Nickson John, alimpongeza Kanal Mnyani kwa kusimamia uanzishwaji bustani hiyo ambayo ni kubwa na itarahisisha wananchi wa mkoa wa Pwani kuona wanyamapori.

Nickson alisema uanzishwaji bustani hiyo ni mwendelezo wa kutangaza utalii kuungana na Rais Samia Suluhu Hassan. Shughuli za kiuchumi katika eneo hilo pia zitakua na kuongeza pato katika kikosi hicho na wakazi jirani.

Athumani Mbega ni mmoja wa wakazi wa Mlandizi ambaye alifika katika bustani hiyo. Alisema kuanzishwa bustani hiyo kutawarahishia kuona wanyamapori karibu na makazi yao, hivyo kupunguza gharama za kwenda kwenye mbuga ambazo ziko mbali.

Katika bustani hiyo mwananchi anapata fursa ya kulisha wanyama na kupiga nao picha bila kupata madhara kutokana na mafunzo wanayopewa wanyamapori hao kabla ya kupelekwa kwenye bustani hiyo.



## Ajali bodaboda yaua mke, yajeruhi mume

**Na Steven William,** MUHEZA

MKAZI wa Masuguru wilayani Muheza mkoani Tanga, Belta Yona, amefariki dunia kwa kugongwa na basi akiwa amepanda bodaboda iliyokuwa inaendeshwa na mumewe.

Tukio hilo limetokea juzi jioni katika eneo la Njia Panda ya Kwamasister Barabara Kuu ya Muheza-Tanga, kwamba mwanamke huyo alikuwa amepakizwa katika pikipiki na mume wake aitwaye John Enock.

Akizungumza na Nipashe, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Almachius Mchunguzi, amethibitisha kutokea kwa ajali hiyo na kusema kuwa ilitokea juzi majira ya jioni.

Kamanda Mchunguzi, alisema wanafamilia hao walipata ajali hiyo wakiwa katika pikipiki wakitokea Tanga Mjini kwenda Muheza, kwamba uchunguzi zaidi unaendelea.

Hata hivyo, alisema walipofika Njia Panda ya kwa Masister waligongwa kwa nyuma na basi la abiria lililokuwa linatokea Tanga kwenda mikoani na kudondokea katika mtaro na kusababisha kifo cha mwanamke huyo ambaye alikanyagwa na gari.

Naye dereva wa pikipiki hiyo, John Enock aliyenusurika katika ajali hiyo, alisema walipofika eneo hilo akiwa na mke wake, aliliona basi nyuma yao na mbele kulikuwa na gari lingine.

Alisema alijaribu kupishana na gari lililokuwa mbele yao, ndipo basi liliwabana na hatimaye kuwagonga kwa nyuma na kusababisha kuanguka pembeni ya barabara na mke wake kutupwa katika uvungu wa basi na kukanyagwa kichwa.



# Mradi uboreshaji miji, majiji wapewa magari mawili

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

HALMASHAURI ya Jiji la Arusha imekabidhi magari mawili kwa Mhandisi wa jiji hilo, Jacob Mwakyambiki, kwa ajili ya shughuli za mradi wa kuboresha miji na majiji, unaotekelezwa katika jiji hilo.

Baadhi ya miradi hiyo ni ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami katika kata mbalimbali za Jiji la Arusha.

Magari hayo yamenunuliwa na serikali, yatakuwa mali ya halmashauri hiyo na Mkurugenzi wa Jiji la Arusha, Jumaa Hamsini, aliyakabidhi kwa Mhandisi wa Halmashauri hiyo.

Akikabidhi magari hayo juzi, Hamsini, aliomba magari hayo yatumike kwa madhumuni yaliyokusudiwa, kwa lengo la kuharakisha mradi huo ili kuwaondolea changamoto wananchi wa Jiji la Arusha.

Katika mradi huo wenye ufadhili wa Benki ya Dunia (WB), magari manne yametolewa na serikali, kati ya hayo mawili yamekabidhiwa jana na mawili yapo njiani kuja.

"Hizi ni nyenzo muhimu sana wakati wa kutekeleza mradi huu, kwa kuwa itarahisisha shughuli za mradi huu, ili ukamilike kwa wakati na kuharakisha maendeleo kwa wananchi, lakini Jiji la Arusha kupitia mapato ya ndani limenunua magari nane likiwamo basi dogo," alisema na kuongeza:

"Leo tumeongeza vitendea kazi kwa ajili ya mradi wetu wa TACTIC, tumekabidhi magari mawili kwa mhandisi wa jiji, kati ya magari manne ya mradi huu na sisi kama halmashauri tumenunua 'Pick up' sita, 'Landcruser' moja na basi dogo moja".

Mbunge wa Arusha Mjini, Mrisho Gambo, alisema mradi wa TACTIC unaenda kujibu kero kubwa za wananchi kwa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami, ikiwamo Barabara ya Engosheratoni, Olasiti na Oljoro.

Alisema mradi huo pia utatekeleza ujenzi wa soko la kisasa la Kilombero na Morombo na ujenzi wa kituo cha kisasa cha mabasi.



Ofisa Raslimali Mwandamizi wa Barrick North Mara, Daniel Paul, akiongea na wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu mkoani Arusha katika kongamano la wanafunzi lililoandaliwa na Taasisi ya AISEC katika Chuo cha Uhasibu cha Arusha mwishoni mwa wiki kwa udhamini wa Barrick. **PICHA: MPIGAPICGA WETU**

# RIVACU yaingiza mil.49.6/- kuuza tani 6 za kahawa

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

CHAMA Kikuu cha Ushirika mkoani Manyara cha Rift Valley Co-operative Union (RIVACU), kimesema kinajivunia kupata tani sita za kahawa sawa na Sh. milioni 49.6.

Kahawa hiyo ni ile iliyovunwa katika shamba la Dareda lililopo Wilaya ya Babati.

Mwenyekiti wa Bodi ya RIVACU, Yuda Sulley, alieleza hayo mwishoni mwa wiki, wakati wa mkutano mkuu wa 34 wa chama hicho.

Sulley, alisema waliuza kilogramu 5,162 za kahawa iliyokobolewa ambayo iliwapatia Sh. mil. 47.4 na kilogramu 550 za kahawa yenye maganda iliyowaingizia Sh. milioni 2.2.

Aidha, alisema fedha hiyo waliyoipata haijawahi kutokea tangu RIVACU ilipoanzishwa.

Mwenyekiti huyo, aliwahakikishia wanaushirika kuwa RIVACU itaendelea kusimamia kwa ufanisi zao la kahawa ili liendelee kuwaingizia fedha nyingi.


Wakati huo huo, mwenyekiti huyo wa RIVACU alichaguliwa kwa kipindi cha pili kupitia mkutano huo kuiongoza bodi ambapo aliibuka mshindi kwa kupata kura 42 kati ya kura 48 zilizopigwa.

Baada ya kutangazwa na Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika mkoani Manyara, Absalum Cheliga, aliiambia Nipashe kuwa atahakikisha wakulima walio kwenye ushirika wanapata uhakika wa masoko ya mazao yao.

Sulley alisema alipopewa nafasi hiyo awamu iliyopita aliikuta RIVACU ina hali ngumu ila tangu aingie wanajiendesha wenyewe bila kukopa taasisi yoyote ya fedha bali wanatumia rasilimali zao.

Wajumbe wengine walioibuka washindi na kutangazwa kuwa wajumbe wa bodi ni Roman Sarwat aliyechaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti kwa kupata kura 30, wajumbe ni Julitha Mziray, Ernest Morembwa, Ramadhan Swalehe, Josephat Aytoo na Erasto John.

Awali, Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika mkoani Manyara, Absalum Cheliga, alisema watu walioomba nafasi za kuwa wajumbe walikuwa 18 ila baada ya mchujo walibaki watu 10 wenye vigezo.



# Majaliwa awashangaa wanaotumia kuni, mkaa

**Na Vitus Audax,** MWANZA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameshtushwa na hali ya wanawake wajasiriamali kuendelea kutumia kuni na mkaa katika kupika, hali inayozidi kusababisha uharibifu wa mazingira na afya.

Kufuatia hali hiyo, ametaka mamlaka husika kuendelea kusimamia kikamilifu utekelezaji wa agizo la kila taasisi inayohudumia watu kuanzia 100 kutumia nishati safi ya gesi ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Alitoa kauli hiyo juzi jijini Mwanza aliposhiriki katika usiku wa tuzo za malkia wa nguvu Kanda ya Ziwa, zilizoandaliwa na Clouds Media Group (CMG).

Majaliwa alifikia hatua hiyo baada ya kushuhudia video iliyokuwa ikimwonesha mshindi wa tuzo ya biashara ya chakula Kanda ya Ziwa, Joyce Kachumita anayehudumia zaidi ya watu 400 kwa siku.

Video hiyo ilimwonyesha wakati akiendelea na shughuli zake za upishi kwa kutumia mkaa na kuni ambavyo vilikuwa vikitoa moshi mkali unaohatarisha afya yake pamoja na mazingira kwa ujumla.

"Nyie wenyewe mmeona mama anayepika vyakula vya watu wengi jinsi anavyohangaika katika moshi wa kuni na mkaa, anapika kwenye chumba chenye moshi mwingi ni vizuri inampatia fedha lakini kwa sasa ndiyo wakati ambao tunatakiwa kubadilika na kutumia nishati safi," alisema.

Aidha, alisema kampeni ya matumizi ya nishati safi inawagusa zaidi wanawake hasusani wajasiriamali kama inavyosimamiwa na Rais Samia Suluhu Hassan ili kuhakikisha matumizi ya kuni na mkaa wa kuchoma iwe mwisho.

"Nyinyi muwe mfano katika utekelezaji wa kampeni hii. Rais Samia Suluhu Hassan, kwa sasa ni kinara wa hamasa ya matumizi ya nishati safi barani Afrika hadi nje ya Afrika," alisema Majaliwa.

Aidha, alisema tayari serikali imeelekeza juu ya taasisi zinazohudumia watu zaidi ya 100 kuanza mchakato wa kutumia nishati safi na kuachana na matumizi ya kuni.

Hivyo, aliwataka wajasiriamali hao kufuata maelekezo hayo ili kuanza kunufaika na matumizi ya gesi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Tuzo hizo, Liliane Masuka, alisema kwa mwaka huu wanatarajia kuziendesha kwa kipindi cha miezi minane na kuwafikia wanawake zaidi ya milioni moja.

Alisema lengo la kufanya hivyo ni kuhakikisha wanaunda ajira mpya, kuinua uwezo mpya wa kibiashara miongoni mwa wanawake pamoja na kutoa mchango katika kukuza pato la taifa.



Meneja wa Shirika la Investing in Children and Society (ICS) la mkoani Shinyanga, Sabrina Majikata (katikati), akikabidhi cherehani ambayo ni moja ya saba wanazopatiwa mabinti wanaoishi katika mazingira magumu wakiwamo waliopewa mimba za ututoni na kuacha masomo, wa pili kutoka kushoto ni Meya wa Manispaa ya Shinyanga, Elias Masumbuko. **PICHA: MARCO MADUHU**.

## Taratibu kuinyanyua Mv. Clarias zinaendelea

**Na Remmy Moka,** SAUT

KAMPUNI ya Huduma za Meli (MSCL) imesema wataalamu wanaendelea na utaratibu wa kuinua Meli ya Mv. Clarias inayohudumia katika Ziwa Victoria, iliyozama wakati imeegeshwa Bandari ya Mwanza Kaskazini.

Akielezea hatua zinazoendelea, Ofisa Uhusiano kwa Umma wa MSCL, Abdulrahman Salim Ally, alisema meli hiyo yenye uwezo wa kubeba abiria 216 na tani 10 za mizigo ilipinduka usiku wa kuamkia Jumapili majira ya saa 11 alfajiri na haikuwa na mali wala mtu.

Alisema hali hiyo ilizua taharuki kwa abiria na jamii wanaotegemea meli hiyo kwa ajili ya usafirishaji wa mizigo, kwamba hadi sasa chanzo cha tukio hilo bado hakijajulikana.

Salim alisema uchunguzi kubaini chanzo cha ajali hiyo utaanza baada ya wataalam kukamilisha shughuli za kuinyanyua na kuipeleka kwenye chelezo, ambapo itafanyiwa marekebisho kwa matatizo yanayoweza kuwa yameikabili pale ilipoanguka.

"Hai hii imesababisha kusitishwa kwa safari za meli hiyo pamoja na meli nyingine ya Mv.Butiama inayofanya safari za Mwanza kwenda Ukerewe ambayo ilizibiwa eneo la kutokea," alisema Salim.

Baadhi ya abiria waliokosa huduma kutokana na meli hiyo kupinduka majini, akiwamo Flora Kila alisema ratiba yake imevurugika na kuingiwa na hofu juu ya hatima ya kufika anakokwenda.

Abiria mwingine Katwale Thomas aliiomba serikali kufanya uchunguzi wa kina juu ya tatizo hilo sambamba na kuvifanyia marekebisho, ili kujihakikishia usalama wa usafari.

# RC ataka wakulima kutochanganya tumbaku

**Na Halima Ikunji,** TABORA

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Paulo Chacha, amewaonya wakulima wa tumbaku mkoani hapa kuacha tabia ya kuchanganya mbaya na nzuri, ambako kunaharibu malighafi hiyo.

Aidha, amesema iwapo wataipanga iliyo nzuri pekee watapata madaraja ya juu na kuyasababishia hasara kampuni ya ununuzi wa zao hilo.

Chacha alitoa onyo hilo wakati akizungumza na wakulima wa vyama vya msingi vya ushirika vya wakulima wa tumbaku, baada ya kutembelea maghala ya Kampuni ya Alliance One Tobacco Limited, (AOTL) kujionea uwekezaji na mwenendo wa soko la tumbaku.

Alisema kuna baadhi ya wakulima wanafanya vitendo vya udanganyifu kwa kuchanganya tumbaku nzuri na mbaya na wengine wanatorosha tumbaku badala ya kuuzia kwenye vyama vyao walivyokopea na kujisajili ambako wanadaiwa madeni yao ya pembejeo.

Alisema uchumi wa Mkoa wa Tabora unategemea kilimo cha tumbaku, hivyo serikali ya mkoa itaendelea kuweka mazingira mazuri ya kuwawezesha wakulima, ambao wengi ni vijana, ili waendelee kuzalisha bila vikwazo vyovyote hasa pembejeo na masoko.

Mkurugenzi wa Uzalishaji wa Kampuni ya AOTL, David Mayunga, alisema uwekezaji wa ujenzi wa maghala ya kuuzia tumbaku mkoani Tabora uliogharimu zaidi ya Sh. bilioni 26.8 ni mkakati wa kukuza uzalishaji wa zao hilo ambalo ni nguzo muhimu ya uchumi wa taifa.

Alisema lengo la kujenga maghala hayo ya kuuzia tumbaku ni kuwa na kituo kimoja cha kuuzia zao hilo tofauti na zamani ambapo walilazimika kuwa na vituo vingi na kusababisha zoezi la ununuzi kuchukua muda mrefu uliokuwa unashusha ubora wa majani yake.

Kwa mujibu wa Mayunga uzalishaji wa tambaku msimu huu umekumbana na changamoto ya mvua nyingi iliyoathiri kiwango cha uzalishaji zikiwamo za kupotea kwa mbolea baada ya kuiweka kwenye mimea, kubomoka kwa mabani ya kukaushia majani ya tumbaku hali iliyosababisha baadhi ya mimea kupoteza ubora na kupungua mavuno.

Alizitaja sababu nyingine iliyosababisha kuathiri ubora na mavuno ni kubainika uwepo wa baadhi ya mbolea ambazo sambuli zake zilionyesha kuwa na kiwango dhaifu.

Meneja Uhusiano wa Kampuni ya AOTL, John Magoti, aliwaomba wakulima kuzingatia taratibu na sheria za uzalishaji wa tumbaku kama wanavyofafanuliwa na maofisa ugani, ili kuepuka hasara kwao na kwa kampuni na kushuka kwa uchumi wa taifa.

Alisema wasipozingatia taratibu na sheria za uzalishaji wa tumbaku watajisababishia hasara kwa tumbaku yao kukataliwa, halmashauri kukosa mapato na uchumi wa taifa kushuka.



Ukurasa 12

**Atikisa Moro akiungana na Rais nishati safi jikoni**



Ukurasa 13

Viboko kwa watoto, wanafunzi adhabu inayozidi kulumbaniwa

Nipashe

TESA

Jumanne Mei 21, 2024

TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI



Ukurasa 14

**Mkono wa taasisi elimu ya juu kuboresha afya ulipoikuna WHO**

ELIMU

NA BEATRICE SHAYO

# Waajiriwa kupoteza haki nyingi kazini kumbe wanapofeli ni hapa

MEI ni mwezi wa kuwaenzi wafanyakazi, tena ukipewa umuhimu zaidi wa kusherehekea Mei Mosi ambayo ni maadhimisho ya siku yao ili kutambua mafanikio na mchango wao kufikia maendeleo.

Katika uwanja wa kazi na ajira suala la mahusiano kazini kati ya waajiri na watumishi ni jambo lisilokwepeka, aghalabu kunyimwa haki na unyanyasaji wa waajiriwa na kuleta migogoro, inayotokea na kuhitaji usuluhishi wa kisheria.

“Ndiyo maana serikali imeunda chombo cha umma cha kutatua migogoro kazini kwa njia za usuluhishi,” anasema ya Mkurugenzi wa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA), Usekelege Mpulla.

Anawakumbusha wafanyakazi kukitumia wanapopata changamoto, akisema ni eneo sahihi la kujibu maswali na matatizo yanayotokea sehemu za kazi.

Akifafanua zaidi, anasema CMA ni chombo cha umma kinachoshughulikia migogoro ya wafanyakazi kwa usuluhishi akisisisitiza kuwa ni taasisi pekee kisheria ambayo ni kimbilio la wafanyakazi wanapovunjiwa haki zao.

Mpulla anayasema hayo wakati wa mahojiano na Nipashe jijini Dar es Salaam, kuhusu masuala ya wafanyakazi ambayo yamepewa kipaumbele hasa wakati huu wa Mei Mosi 2024.

Anataja baadhi ya mambo kuwa ni kuachishwa kazi bila kufuata taratibu na wala kuwapo sababu za utoshelezi, kutokulipwa mishahara ama kupewa chini ya kiwango cha kima cha chini kilichopangwa kisheria.

“Kuna mengine kama madai ya likizo na kiinua mgongo, hivyo wafanyakazi wafahamu kuwa CMA ndilo kimbilio ili kupata haki. Kwa kutambua umuhimu wa wafanyakazi na waajiri ambao ni wazalishaji kwa lengo la kukuza uchumi wa taifa.”

**MIKAKATI**

Anasema CMA ni taasisi huru inayoshughulika na utatuzi wa migogoro ya kikazi Tanzania Bara kati ya waajiri, waajiriwa na vyama vya wafanyakazi na kwamba ili kutumiza azma hiyo ni lazima kwenda na wakati au kidijitali.

“Moja ya mkakati wetu ni kutumia mtandao kuruhusu wafanyakazi watakaokuwa na kesi kuziwasilisha kwa njia ya mtandao. Tunakuja na mfumo wa Online Case Management System (OCMS). Shauri tutalifanyia kazi na mwajiri atahojiwa kuhusiana na madai yaliyowasilishwa.” Anafafanua kuwa wanalenga kumaliza migogoro inawagusa wafanyakazi kwa haraka ili wasitumie muda mwingi kwenye kesi bali utumike zaidi kuzalisha.

Mipango ipo katika hatua mbalimbali na tayari wameanza kusimika mifumo itakapokuwa tayari utawawezesha hata wale walio mbali kuhudumiwa bila ucheleweshaji.

“Ina maana akipata kesi kama ana simu janja ataingia katika mtandao na kuwasilisha taarifa zake kwenye mfumo zitatufikia, tutasajili kesi na kuweka utaratibu wa kuanza kutatua migogoro,” anasema Mpulla.

Anasema katika hatua nyingine ukishasajili kesi watakuwa na uwezo wa kutoa taarifa kwa aliyeshtakiwa kwa kuwa mfumo utakuwa na taarifa kutoka kwa aliyefungua shauri.

Anaeleza kuwa atapata taarifa ya kuhusu shauri kufunguliwa dhidi yake baada ya hapo taratibu za kupanga tarehe ya kuanza kusikilizwa pasipo ulazima wa kufika ofisini zitaanza.

Anawaambia wadau kuwa mfumo wa OCMS unatarajia kuanza mwishoni mwa mwezi ujao na kwa sasa upo kwenye hatua ya majaribio ya watumiaji ambao unatarajia kuanza Mei mwaka huu.

“Kwa sasa tunachokifanya ni kuhakikisha mifumo inasomana kama mlivyomsikia Rais Samia Suluhu Hassan, akisisitiza hilo. Mahakama na taasisi mbalimbali tunazofanya kazi za kufanana lazima mifumo isomane ndicho tunachokifanya baada ya kukamilisha tunaenda katika majaribio ya watumiaji,” anasema.

Mkurugenzi Mpulla anasema kuna mkakati na maandalizi yake yanafanyika ili kuwafikia walio mbali kwa maana migogoro itakayokuwa imesajiliwa kutoka maeneo ya mbali watairatibu na kuipangia tarehe kisha msuluhishi ama muamuzi wa migogoro atakwenda waliko.

“Mfano mwezi huu tumepokea kesi fulani kutoka wilaya moja, tutakwenda kuwajulisha siku tunayokuja lengo kuwapunguzia gharama tutawafuata waliko ... ni kurahisisha na kuwasogezea wananchi huduma karibu.”

**UELEWA TATIZO**

Mpulla anaeleza kuwa moja ya changamoto zinazosababisha wafanyakazi wengi kupoteza haki zao ni uelewa mdogo katika kuwasilisha migogoro yao ndani ya muda uliowekwa kisheria.

“Wafanyakazi wanatakiwa kutambua changamoto kadhaa ambazo zinasababisha wengi kupoteza haki zao ni vyema wakazitambua. Mosi ni uelewa mdogo wa wafanyakazi wengi kujua ni wapi pa kuipeleka,” anasema Mpulla.



Mkurugenzi wa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi, Usekelege Mpulla. **PICHA: MTANDAO**

INAENDELEA UK.13

ELIMU
NA BEATRICE PHILEMON

JANETH MAKWENJULA

# Atikisa Moro akiungana na Rais nishati safi jikoni

RAIS Samia Suluhu Hassan, ni championi wa nishati safi ya kupikia na ulinzi wa mazingira, aliye mstari wa mbele kuhimiza nishati safi jikoni ili kuboresha maisha ya Watanzania hasa kinamama.

Mbali na hilo ni kinara kuhimiza wananchi kuachana na nishati chafu kama vile mkaa, kuni, mafuta ya taa na kinyesi cha wanyama ambayo huleta athari za kiafya, kimazingira, kiuchumi na kijamii. Ni wazi kuwa Tanzania ni kubwa na inahitaji elimu ya jiko lisilochafua mazingira wala afya kumfikia kila mwanamama na umma pia, anasema Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake (UWT) Wilaya ya Ulanga mkoani Morogoro Janeth Makwenjula, anayeunga mkono matumizi ya nishati safi.

Anawafundisha na kuwahamasisha wanawake Wilaya ya Ulanga wakiwamo wajasiriamali, mama na babalishe na wafanyabiashara wenye migahawa kuanza kutumia gesi ya mitungi LPG.

Anasema hadi sasa amehamasisha kinamama wa kata zote 21 za Wilaya ya Ulanga jinsi ya kutumia jiko la gesi na pia kupanda miti katika maeneo yao.

"Hivi sasa mwamko wa matumizi ya majiko ya gesi katika kata ya Milola unaanza kuwa mkubwa wanawake wengi wanajitokeza kujifunza pia wanaume wamehamasika kuzinunulia familia zao majiko ya gesi..." anasema.



Janeth Makwenjula (kulia), akikabidhi mitungi ya gesi yenye jiko kwa wanawake wafanyabiashara migahawani. **PICHA: UWT**

### MBINU ANAZOTUMIA

Janeth anasema amekuwa akitumia vikao vya umoja wa kinamama kuelimisha umma matumizi ya nishati safi vijijini, kata na wilaya.

Anasema anakusudia kuleta mabadiliko maana kwa sasa mahitaji ni mengi vijijini, wananchi wanazungumzia umuhimu wa mitungi lakini bei ipunguzwe kwa mitungi na gesi kwasababu wananchi wanategemea kilimo cha mpunga na hawana kipato cha uhakika.

"Baada ya kuona mwamko wa wanawake kuanza kuhitaji majiko ya gesi kuwa mkubwa, nimemuomba msaada mbunge wa viti maalumu mkoa, Christine Ishengoma, majiko ya gesi 67 ili niweze kufundishia wanawake na mengine kugawa kwa viongozi wa kata ili wanisaidie kuelimisha wanawake katika maeneo yao."

"Namshukuru sana Mama Ishengoma kwa sababu wakati wa kutoa elimu nilifanikiwa kugawa majiko ya gesi 12 kwa mamalishe katika kata ya Mahenge, majiko Milola na 50 kwenye kata zote 21 za wilaya ya Ulanga kwa wenyekiti na makatibu wa UWT wa kila kata kila moja ikipata majiko mawili," anasema.

Mbunge wa Ulanga, Salim Hasham, anamwongezea majiko 200 ya gesi kwa ajili ya kuendelea kuhamasisha kinamama kwenye vijiji, tarafa, kata mkoani humo kuhusu matumizi ya nishati safi.

"Nimegawa majiko haya katika kata ya Mahenge, Lupilo, Ruaha na Mwaya, lengo ni kuhamasisha wanawake kuacha kutumia kuni, mkaa na kutunza mazingira, zaidi ya wanawake 200 wamenufaika na msaada huu."

### MAZINGIRA BORA

Mbali na hilo, anahamasisha kinamama kuhifadhi wa mazingira na upandaji wa miti kwenye sehemu wanazoishi ili kuhifadhi mazingira, kuzuia mmomonyoko wa udongo hasa sehemu za milimani ambapo hivi sasa miti mingi imekatwa na wafugaji kwa ajili ya kilimo, kuchoma mkaa na kuni.

Hadi sasa wanawake wamepanda miti 52 katika kata ya Milola, miti 100 katika zahati ya Mavimba na mingine 1,000 katika kata ya Mahenge.

"Nimeamua kuanzisha kampeni hii baada ya kuona hali ya ukataji misitu katika wilaya ya Ulanga ni kubwa, wafugaji wanakata kupata malisho, kuni, kuchoma mkaa na shughuli za kilimo," anaelezea.

Pia athari za mazingira ni kubwa, hivi sasa msitu uliopo kwenye mlima wa Ndololo miti mingi imekatwa, wafugaji wanachoma mkaa ba eneo linaelekea kuwa jangwa, anasema.

"Wakati wa mafunzo niliwafundisha kinamama kupanda miti kwenye eneo la majumbani mwao, kwenye viwanja, mashamba yao ya kilimo kwa ajili ya kuzuia upepo na pia kwenye misitu na mashamba ya vijiji na kila kijiji kimepewa miche ya kupanda wanayopata kutoka Halmashauri ya wilaya ya Mahenge.

Pia hivi sasa wamepanda miche ya miembe 68 kwenye eneo la ekari mbili katika Kijiji cha Chikuti kilichopo jirani na Milola, anasema Janeth.

Akizungumza na Nipashe Mwenyekiti wa Kijiji cha Milola, Harun Mholoholo anakiri kuwa baadhi ya wananchi wameanza kutumia majiko ya gesi lakini bado ni wachache.

Anaomba serikali au wafanyabiashara wanaouza majiko ya gesi wasogeze huduma hii karibu na wananchi katika kata au au vijiji ili iwe rahisi kwa kinamama na wananchi wengine kupata majiko hayo kwa urahisi na kwa bei nafuu.

## Waajiriwa kupoteza haki nyingi kazini kumbe wanapofeli ni hapa

INATOKA UK.11

Aidha, anasema wengine wanaachishwa kazi wanakwenda kulalamika kwa Mkuu wa Mkoa ama Mkuu wa Wilaya na kujikuta akichelewa kupata haki zake kwa kuwa ameenda sehemu ambayo sio sahihi.

"Unaachishwa kazi unakwenda kulalamiko kwa mbunge, kwa waziri ama kwa mkuu wa mkoa kwa ufupi wanawasilisha malalamiko kwa wanasiasa kisheria hao hawana mamlaka wanapokwenda huko wanajichelewesha wenyewe na kujikuta wamepoteza haki zao kwa kwa sababu sheria inaelekeza kesi ya kuachishwa kazi ifunguliwe kwenye CMA ndani ya siku 30," anakumbusha Mpulla.

Anaongeza: "Unamfuata mwanasiasa anamwambia anaweza kusema nisubiri au yupo bungeni au kwenye ziara halafu siku 30 zimekisha kwetu kesi inafutwa kwa sababu ipo nje ya muda."

Mpulla anasema hiyo ni moja ya changamoto kubwa wengi wanaopoteza haki zao kwa sababu ya kutokuwasilisha migogoro ndani ya wakati uliowekwa kisheria.

Anasema ukiachilia mbali kuachishwa kazi, migogoro mingine sheria inataka iwasilishwe ndani ya siku 60, hivyo hawapaswi kwenda sehemu yoyote bali kufika CMA.

### KUMALIZA KESI

Mpulla anasema mkakati wao wa kwanza ni kuhakikisha kesi ya usuluhishi inaisha ndani ya siku 30 tangu kufunguliwa muda uliopo kisheria.

Anasema mkakati wao wa ndani wamejiwekea siku 21 kwa kutambua umuhimu wao na endapo ikatokea usuluhishi ukashindikana katika uamuzi baada ya kusikiliza uamuzi unatakiwa utoke ndani ya siku 30 ambayo ni hukumu.

### KESI ZINAZOSAJILIWA

Akizungumzia idadi ya kesi wanazozipokea, Mpulla anasema inategemea na mwaka utakavyokuwa na kwa makadiri kwa mwaka kesi zaidi ya 10,000 zinasajiliwa CMA.

ELIMU

NA JALIWASON JASSON, MANYARA

# Viboko kwa watoto, wanafunzi adhabu inayozidi kulumbaniwa



Wadau wanapinga ukatili kama huu unaozidi adhabu. **PICHA: MTANDAO**

ADHABU ya viboko hutumika kuwakanya na kuwarudi watoto na wanafunzi shuleni. Ni kwa nadra walimu, wazazi au walezi wakaacha kiboko kwenye malezi.

Lakini ipo shuleni msingi na sekondari ili kuwaweka watoto au wanafunzi kwenye mstari darasani lakini pia suala la nidhamu kiboko hakiwezi kuwa mbali.

Gumzo la adhabu hii ni la siku nyingi na kila wakati linaibuka, mathalani wazazi na walezi wilayani Babati mkoani Manyara wana haya.

Musa Rehan, anaungana na kundi la wanaokubali adhabu ya viboko iendelee kwenye malezi na makuzi ili kurekebisha nidhamu ya mtoto au mwanafunzi.

Ana ushuhuda kuwa akiwa mwenyekiti wa kamati ya Shule ya Msingi Oysterbay iliyopo Babati mwaka 2005 alisimamia kiboko kidumu.

"Mtoto kuchapwa ni kukosolewa, kunyooshwa na kurekebishwa ambao hawachapwi ndiyo wanakuwa mateja, wavuta bangi na walevi."

Akiwa mwenyekiti wa kamati ya shule alipokea wajumbe wa tume ya kuangalia utoaji wa adhabu shuleni ambapo ilikuwa inataka mwalimu mkuu aruhusu kuchapa, aliigomea kwasababu mwalimu yeyote anachapa kwa nia ya kurekebisha na kujenga wala si kuumiza.

Rehan anasema watoto wasipochapwa ni kuwalea kizembe na kuongeza: "Sioni sababu mwalimu akitaka kumwadhibu mwanafunzi aombe ruhusa kwa mwalimu mkuu, yote haya yanaleta kudharauliwa na wanafunzi," anaonya Rehan.

Mkazi wa Mtaa wa Komoto, John Tango, anaungana na Rehen akisema hakuna tatizo bali walimu wanaochapa kupita kiasi hata kuumiza wanakosea.

Tango anasema watoto hata nyumbani wazazi na walezi wanawaadhibu ila kwa kiwango cha chini kisichokuwa na madhara kiafya na kisaikolojia.

Mkazi wa Kijiji cha Bermi Adelina Paul, anaipinga kwa maelezo kuwa inasababisha baadhi ya wanafunzi kuikataa shule.

"Ukifatilia wengi walioacha shule chanzo ni kiboko," anasema Adelina na kushauri iwepo sheria ya kuadhibu wanaochapa kiboko kupita kiasi, iwahusu walimu au wazazi.

Mkazi mwingine wa Kijiji cha Matufa Halima Halfan anasema adhabu ya viboko inawaumiza wanafunzi kuwajengea woga na kusababisha washindwe kujiamini.

### KUISHIWA MBINU

Meneja mradi na elimu wa Shirika la So They Can (STC), Grace Swai, anasema viboko vimepitwa na wakati na anayetumia adhabu hiyo ameishiwa mbinu.

"Ukimchapa mwanafunzi unamweka mbali na wewe ili asijifunze zaidi. Wapo watoto wanalea familia, wanatoka mbali na shule ila walimu hawawasikilizi anawaadhibu," anasema Grace.

Anataja sheria ya elimu ya mwaka 1978, inayoagiza kuwa mwalimu mkuu ndiye anatakiwa kutoa ruhusa ya kuchapa viboko tena kwa maandishi.

Grace anatahadharisha walimu na kutumia viboko kuwa watoto wengine wakichapwa wanazimia au kupoteza maisha hivyo wawe makini au waiepuke adhabu hiyo.

Ofisa Mradi wa Sauti Yangu, wa Shirika la So They Can, Peter Nelson, anasema mradi wao unawajengea uwezo wanafunzi kujua haki zao, kusema vitu wanavyovipenda au wasivyovipenda vinavyofanywa na walimu shuleni.

Nelson anasema wamewafikia wanafunzi wa shule za msingi kuanzia darasa la awali mpaka darasa la saba 17,000 na wa sekondari 21,000.

Aidha, anasema walimu zaidi ya 300 wamewapatia elimu ya mbinu za kuepuka kutoa adhabu ya viboko.

Licha ya mbinu hiyo anasema walimu wanatembelea shule za mchepuo wa Kingereza kujifunza namna ya kutoa adhabu bila kutumia viboko akitoa mfano kuwa mwanafunzi anaweza kupewa kadi, kunyimwa ruhusa ya kucheza na wenzake.

Ofisa huyo anasema kabla ya STC kuanza kutoa elimu kwa walimu shule nyingi walikuwa wakiwapiga viboko lakini kwa sasa mambo yamebadilika.

Anaongeza kuwa awali walimu wa kiume walikuwa wanawachapa wanafunzi wa kike viboko kwenye makalio licha ya kwamba ni kinyume na utaratibu.

Nelson anasema serikali iendelee kutoa mafunzo vyuo vya ualimu na walimu waondoe fikra mgando za ya kuendeleza viboko.

Mkuu wa Programu, Godfrey Bonaventure, kutoka Shirika la HakiElimu anasema hali halisi ya matumizi ya viboko na uzoefu wa kutokuvitumia inaonyesha wengi wamezoea kuchapwa.

Anafafanua kuwa asilimia 87.9 ya watoto shuleni wamezoea kuchapwa na asilimia 90 wanapigwa, akiuita ukatili waliouzoea.

Boniventure anasema utafiti wa HakiElimu unaonyesha kuwa asilimia 89.0 wamezoea kuchapwa shuleni, wakati 10 wamezoea kuchapwa nyumbani akisema asilimia 37.1 wanachapwa na ni aina ya adhabu inayotumiwa na walimu kila siku vijijini.

> Ukimchapa mwanafunzi unamweka mbali na wewe ili asijifunze zaidi. Wapo watoto wanalea familia, wanatoka mbali na shule ila walimu hawawasikilizi anawaadhibu.

Anaongeza kuwa asilimia 16.3 ni aina ya adhabu inayotumiwa na walimu mijini kila siku.

Utafiti huo unaonyesha mataifa ya Afrika yanayochapa viboko ndani ya miezi 12 ikiwamo Tanzania yenye asilimia 43.

Uganda 35, Malawi 25, Kenya 21, Nigeria 19, Zambia tisa, Lethoto nne na Zimbabwe nne.

Katika utafiti huo wanafunzi wanasema: "Nikichapwa viboko napata maumivu makali yananifanya nisiwe na utulivu darasani. Yaani sitamwelewa mwalimu kabisa"

"Viboko vinatufanya tuwaogope walimu na kushindwa kuomba msaada unapohitajika" "Siwapendi walimu wanaotumia viboko."

### ADHABU CHANYA

Utafiti huo umezungumzia adhabu chanya kuwa adhabu kali ilikuwa asilimia mbili, kazi za ziada za mtaala asilimia 18, kazi za shuleni kufanyia nyumbani asilimia 10, kumwongoza na kumshauri asilimia 26 na kusafisha madarasa asilimia 44.

Taarifa ya Mtandao wa Elimu Tanzania(TENMET), ya Septemba 2018 ililaani adhabu ya viboko.

TENMET inawakumbusha walimu na wananchi kuwa muongozo wa kutoa adhabu mashuleni chini ya kifungu cha 61(1)(v) cha sheria ya elimu sura ya 353 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2002 inaeleekza utoaji wa adhabu hiyo.

TENMET inasema mtoto ana haki ya kulindwa, kuendelezwa, kuishi, kushirikishwa na kutobaguliwa.

Mshauri wa malezi makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto Davis Gisuka kutoka Shirika la Children Incrossfire (CIC), anasema walimu wanaotoa adhabu ya viboko kwa wanafunzi wa chekechea wanawaharibu makuzi ya ubongo.

Gisuka anasema wakiwa wanachapwa viboko akili yao itakuwa chini na hata wakienda shule hawatAweza kujifunza vizuri na kuelewa.

Aliyataja madhara wanayoweza kuyapata wanafunzi wa chekechea kuwa ni wanafunzi wote kuumia, kuharibika kisaikolojia na kuwajengea woga.

Vile vile anasema walimu wanaocharaza bakora wanaharibu mahusiano yao na wanafunzi na wengine kuwafanya wachukie shule.

ELIMU

NA CHRISTINA MWAKANGALE

# Mkono wa Taasisi Elimu ya Juu kuboresha afya ulipoikuna WHO

JUHUDI za kuboresha huduma za afya ya Mtanzania zinazofanywa na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS) na Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE), zimeligusa Shirika la Afya Duniani (WHO) linalotangaza kuzitambua na kuziendeleza.

Utambuzi huo unakihusisha pia Chuo Kikuu Mzumbe pamoja na mashirika mengine 11 ya kitaifa na kimataifa yanayofanya juhudi za kuboresha afya ya Mtanzania, kwa kugusa mifumo ya kutoa huduma hizo.

Katika kuendeleza juhudi hizo, WHO inaingia makubaliano na taasisi hizo na kuafikiana kufanyakazi zaidi na kuleta mapinduzi ya kumpa afya bora kila mwananchi.

Mkuu wa Chuo cha DUCE, Profesa Stephen Maluka, akizungumza na Nipashe, baada ya kusaini makubaliano na WHO, jijini Dar es Salaam hivi karibuni anasema moja ya mambo yaliyofanywa na taasisi hiyo ni utafiti wa uwajibikaji wa vyombo vya kusimamia utoaji huduma za afya.

Itakumbukwa kuwa mwaka 2022 katika mradi wa kutathmini uwajibikaji wa kamati za usimamizi wa vituo vya afya na bodi za afya za halmashauri ulifanyika utafiti katika wilaya za Mbarali mkoani Mbeya na Handeni Tanga na kubainika kuwa kulikuwa na kukosekana uwajibikaji, anasema Profesa Stephen Maluka.

Akizungumza na Nipashe baada ya kutambuliwa na WHO, Profesa Stephen Maluka, anasema ushiriki wa chuo kwenye tafiti mbalimbali umekipa heshima hiyo na kukifikisha kwenye hatua hiyo ya kujivunia.

Anaongeza kuwa DUCE inaratibu mradi wa miaka mitatu ulioanza 2021 hadi 2024 unatarajia kuongeza uwajibikaji wa kamati za usimamizi wa vituo vya afya na bodi za afya za halmashauri.

Anakumbusha kuwa awali utafiti huo uliozihusisha wilaya za Mbarali na Mji wa Handeni ukiwashirikisha wananchi 1,184 na kubaini kuwa asilimia kubwa ya wananchi hawajui iwapo kuna kamati za usimamizi wa vituo vya afya pamoja na bodi za afya za halmashauri, ambazo zipo kwa ajili ya kusimamia utoaji wa huduma kwenye vituo na hospitali za wilaya.

Profesa Maluka, akiwa mtafiti kiongozi anasema: "Utafiti huo ulilenga mambo mawili makubwa, kutathmini uelewa wa wananchi kuhusu utendaji kazi wa kamati za usimamizi wa vituo vya afya. Pamoja na kutathmini uwajibikaji wa kamati za usimamizi wa vituo vya afya na bodi za afya za halmashauri."




Viongozi wa taasisi zilizotambuliwa na WHO kuboresha afya. **PICHA: WHO**

> Asilimia 85.3 ya wananchi walikuwa hawajui kama kuna kamati hizo wakati asilimia 96.5 walikuwa hawana habari za uwepo wa bodi za afya za hospitali za halmashauri.

Anasema katika kuleta mabadiliko na kuongeza uelewa miongoni mwa jamii, matokeo ya utafiti yaliwasilishwa kwa wadau kuanzia wananchi, wajumbe wa kamati, bodi, watendaji wa serikali kama vile waganga wakuu wa wilaya hizo na wakurugenzi.

"Asilimia 85.3 ya wananchi walikuwa hawajui kama kuna kamati hizo wakati asilimia 96.5 walikuwa hawana habari za uwepo wa bodi za afya za hospitali za halmashauri."

Aidha anasema asilimia 88.3 ya wananchi waliohusishwa walibainika kuwa hawakuwahi kusikia kuhusu uchaguzi wa wajumbe wala kushiriki kuwachagua wajumbe wa kamati na bodi hizo ili kusimamia huduma.

"Kama wananchi hawajui kuna kamati za usimamizi maana yake hata uwajibikaji wa hizi kamati na bodi ni changamoto." Anaeleza.

Kutokana na uelewa wa wananchi kuwa mdogo, Profesa Maluka anasema pia utafiti ulionesha asilimia 96.7 hawajawahi kupata mrejesho wowote kutoka kwenye vyombo hivyo vya usimamizi na kudhihirisha kuwa uhusiano kati ya kamati, bodi na wananchi ni mdogo.

Baada ya matokeo hayo, watafiti walitoa elimu kwa wadau mbalimbali ili kuwafikia wananchi kuhusu majukumu na utendaji kazi za kusimamia vituo na hospitali ili kuongeza uelewa na uwajibikaji wa mamlaka hizo za usimamizi. Aidha, anasema lengo ni kuimarishwa, ili zisiwajibike kikamilifu kwa watu na kusimamia fedha zinazowekezwa kwenye vituo vya afya na hospitali za wilaya kote nchini.

Akizungumzia makubaliano na WHO, anaeleza kuwa yatafanikisha utoaji wa elimu kwa wananchi na wadau wa afya, kuboresha elimu ya lishe, mifumo ya utoaji huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto pamoja na kinga, kadhalika kutekeleza vipaumbele vya serikali," anasema Profesa Maluka.

Profesa Peter Kamuzora, kutoka Taasisi ya Taaluma za Maendeleo UDSM, anasema hatua ya mabadiliko kwenye sekta ya afya imewezesha wananchi kushirikishwa katika mipango ya kiafya ya mwaka na kutoa maamuzi katika huduma.

Anasema hilo linafanyika kupitia wawakilishi wao kwenye kamati za usimamizi wa vituo vya afya ngazi ya zahanati, kituo cha afya na hospitali na bodi za huduma za afya za halmashauri.

Profesa Kamuzora, anataja hayo anapowasilisha mada kuhusu chimbuko na mabadiliko kwenye sekta ya afya nchini, kwenye mafunzo ya siku mbili yaliyohusisha wajumbe, wenyeviti, makatibu wa bodi na kamati hizo pamoja na maofisa watendaji kata wa wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya.

"Matokeo na maendeleo katika utekelezaji wa mabadiliko katika sekta ya afya, wizara inaendelea kushughulikia uanzishwaji wa bima ya afya kwa wote, aidha inaendelea kushirikisha sekta binafsi na wadau wote katika kuimarisha huduma hizo," anafafanua.

Anaongeza: "Serikali imezifanyia mapitio sheria mbalimbali na kuanzisha nyingine, mfano, sheria ya bima ya afya ya taifa (1999) na sheria ya mfuko wa afya ya jamii (2001), pia imebuni vyanzo vingine vya mapato, ili kugharamia huduma za afya papo kwa papo..."

Mwakilishi Mkazi wa Shirika la WHO, Dk. Charles Sagoe-Moses, anasifu wadau wote, akisema kuwa makubaliano na taasisi hizo yametambua mchango mkubwa unaofanywa na mashirika mbalimbali kwenye sekta ya afya, kuhakikisha hakuna anayeachwa kando.

"WHO inatambua thamani na kinachofanywa na taasisi hizi, kuboresha huduma za afya, hususan kwenye ajenda ya afya kwa wote," anasema Dk. Charles na kwamba makubaliano hayo yatajikita katika kuimarisha mifumo ya afya, kinga dhidi ya magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza (NCDs), ya mlipuko na kuhimiza mtindo bora maisha.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Baraza la Taifa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NACONGo), Rachel Chagonja, akiweka saini pamoja na WHO, kwa niaba ya mashirika 11, anasema makubaliano hayo yanabainisha nia ya kuongeza wigo wa huduma zinazomfikia kila Mtanzania.

Anafafanua kwamba, makubaliano yanawiana na ya shirika hilo, kwenye sekta ya afya, kwa kuwajengea uwezo wataalamu, kufanya utafiti na kuimarisha mifumo, huduma za afya ngazi ya jamii.

Katika utambuzi huo pamoja na DUCE, Shirika la Afya Duniani pia limevitambua vyuo na taasisi kadhaa zikiwamo Taasisi ya Catholic Relief Services (CRS), Doctors with Africa (CUAMM), SIKIKA, Chuo Kikuu Mzumbe, Tanzania Health Summit (THS) na AMREF HEALTH AFRICA Tanzania.

Wengine ni International Rescue Committee, Ifakara Health Institute (IHI), Raising Up Friendship Foundation (RUFFO) pamoja na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS).



## TRA yajivunia makusanyo kupaa miaka 3 ya Samia

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Dodoma umeongeza wastani wa ukusanyaji kodi kutoka Sh.bilioni 15.19 hadi Sh.bilioni 18. 71 katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi kuhusu mafanikio ya mamlaka hiyo jijini hapa, Meneja wa TRA, Mwita Ayubu, alisema mafanikio hayo ya makusanyo yametokana na uboreshaji wa uhusiano kati yao na walipakodi.

Alisema kuwa mwaka 2021 Mkoa wa Dodoma ulikuwa na wafanyabiashara 3,812 wanaotumia mashine ya EFD, hivi sasa wameongezeka na kufikia 9,367 ikiwa ni ongezeko la wafanyabiashara 5,555.

"Mengine yaliyowezesha kupanda kwa kiasi hicho cha fedha cha ukusanyaji ni ongezeko la uwekezaji na ukuaji wa shughuli za kiuchumi ikiwamo uzalishaji viwanda na sekta za ujenzi na usafirishaji na uhamasishaji kwa kupitia elimu kwa mlipakodi," alisema.

Alibainisha kuwa pia ongezeko la matumizi ya mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika usimamizi wa kodi kutoka kwa wananchi kwa kulipa kodi kwa hiari, kuongezeka kwa hamasa ya ulipaji kodi kutoka kwa wananchi kwa kuona matumizi sahihi ya kodi wanazolipa.

Hivyo, aliwasisitiza wafanyabiashara kutumia mashine za EFD kutokana na kuwapo kwa faida kama vile uboreshaji wa kumbukumbu za biashara kwa njia za elektroniki ambayo ni salama na ya kuaminika.

Hata hivyo, alisema mamlaka hiyo inakabiliana na tatizo la kuongezeka kwa wimbi la matumizi ya stempu za kielektroniki za kughushi kwa walipakodi, hali inayosababisha upotevu mkubwa wa mapato.

# Tume yataja sababu za kuletwa roboti Eunice

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SIKU chache baada ya roboti Eunice kuwa gumzo katika mitandao ya kijamii, Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya TEHAMA nchini, Dk. Nkundwe Mwasaga, amesema lengo la kuleta roboti hiyo ni kuimarisha ubunifu wa kidigitali katika kukuza uchumi wa taifa.

Akizungumza na Nipashe, Dk.Mwasaga alisema teknolojia ya roboti inaweza kusaidia katika majukumu mbalimbali ikiwamo ajali inapotokea.

"Huu ni ubunifu ambao tumeufanya kati ya Tume ya TEHAMA na wizara yetu, kwa sababu wizara yetu ndio inayosimamia mambo yote ya kidijitali kuhakikisha kwamba Tanzania inakuwa shindani na inakuwa katika viwango vya kidunia vya mambo hayo," alisema.

Aliongeza: "Tumefanya mambo mengi ambayo mmeyasikia, tumepeleka mawasiliano sehemu mbalimbali ikiwamo kujenga mkongo, sasa, tunaenda katika teknolojia ibukizi katika hizo, teknolojia ambayo ina jina kubwa sana ni akili mnemba na mambo ya roboti kama mnavyoiona," alisema.

Alibainisha kuwa tume ina mpango wa kununua maroboti mengine ambayo watakuwa wanafanya kazi na vyuo mbalimbali na watu wengine.

"Kazi kubwa ni kukuza ubunifu wa kidijitali na maroboti kama haya yana matumizi mengi ya kijamii, tulichokifanya hapa, tumemleta huyu roboti na roboti kama mnavyofahamu anaitwa Eunice na yeye amewekewa teknolojia za kisasa sana, anaweza kuona na anaweza kusikia na anaweza kufanya mazungumzo na watu," alisema.

Alisema jukumu lao kwa sasa ni kutambua roboti zipi zitatumika maeneo ya viwandani, ni roboti zipi ambazo zinatumika katika maeneo ya super market, roboti zipi zinatumika katika maeneo ya ajali.

Aliongeza: "Lakini, ninataka kuwatoa wasiwasi watu kuhusu kupoteza kazi, siyo kweli. Roboti zitatufanya kufanya shughuli zetu kwa tija zaidi kwa mfano kama ulikuwa unafanya uzalishaji kwa wiki moja sasa hivi unaweza kufanya kwa muda mfupi zaidi".



Mwendesha baiskeli akiwa amepakia madumu yaliyozidi idadi kandokando ya barabara ya mabasi ya mwendeo kasi, Magomeni jijini Dar es Salaam jana wakati akisubiri kuvuka.**PICHA: JUMANNE JUMA**

## Majaliwa akipongeza OUT utoaji mafunzo TEHAMA

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amekipongeza Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) kwa kutoa mafunzo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwa watu wenye ulemavu.

Alitoa pongezi hizo mwishoni mwa wiki baada ya kutembelea banda la chuo hicho kwenye maonesho ya TEHAMA yaliyofanyika viwanja vya Bunge jijini hapa.

Majaliwa alikitaka chuo hicho kufanya jitihada za kujitanua katika mafunzo hayo ya TEHAMA kwa walemavu ili kuwafikia hata waliopo katika sehemu mbalimbali za nchi.

Alisema hatua hiyo itatanua wigo wa matumizi ya TEHAMA kwa makundi hayo ya walemavu.

Naye Mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu ya Uongozi na Menejimenti katika Teknolojia wa OUT, Dk. Catherine Mkude, alisema maonesho hayo yamekuza wigo wa ufahamu wa elimu ya TEHAMA kwa walemavu kwa viongozi na wabunge ambao watakwenda kuwafahamisha wananchi katika majimbo yao.

Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya TEHAMA, Dk. Mkundwe Mwasaga, alisema uwepo wa maonesho haya umekuza nafasi za mashirikiano baina ya taasisi ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za TEHAMA kwa taasisi hizo kuangalia maeneo muhimu wanayoweza kushirikiana.

## CWT yataka waraka upandishaji vyeo kuharakishwa

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

CHAMA cha Walimu Tanzania (CWT) kimeitaka serikali kuharakisha mchakato wa kutoa waraka wa kupandishwa vyeo watumishi wa umma.

Mwenyekiti wa CWT Mkoa wa Singida, Hamisi Mtundua, alisema hayo jana wakati wa Mkutano Mkuu wa Umoja wa Walimu Kanda ya Kati na Kaskazini (NOCETEC), ambao uliwajumuisha walimu na viongozi wa CWT kutoka mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Dodoma na Singida ambao umefanyika mjini Singida.

"Walimu hawa ili waendelee kuwa na nyuso za furaha ni lazima wapewe kile wanachostahili kukipata, mpaka sasa tulitakiwa tuwe tumepewa waraka wa kupandishwa vyeo lakini hadi sasa hatujapata na kwa mujibu wa taratibu cheo kinapaswa kupanda Julai Mosi lakini tumecheleweshewa," alisema.

Mtundua alisema suala la kikokotoo bado walimu hawajamalizana na serikali na kwamba wana imani kubwa na serikali italifanyia kazi suala hilo, kwa kuwa kile wanachokipata walimu hakitoshelezi.

Naye Rais wa CWT, Leah Ulaya, alisema walimu wana kauli mbiu yao inayoitwa 'wajibu na haki' ambayo ili kutimiza wajibu wao ni lazima kuwa na viongozi mahiri.

"Ili tuweze kutimiza wajibu wetu kuna mambo matatu ya kuzingatia ambayo ni, mosi, kuwe na uhusiano wa kati ya pande mbili yaani mwajiri na mwajiriwa na yawe mahusiano mazuri ambayo yatafanya daraja kati ya mwajiriwa na ofisa utumishi," alisema Ulaya.

Alisema kuwa walimu wanatamani kuona mambo yao yote wanayohitaji wayapate kwa wakati na pia kuwepo kwa mshikamano baina yao na serikali.

Naye Katibu wa CWT Mkoa wa Singida, Digna Nyaki, akisoma risala ya walimu kwa mgeni rasmi alisema walimu wengi bado hawajalipwa madeni yao licha ya kwamba yamehakikiwa tangu mwaka 2017.

Pia alisema tatizo lingine linalowakabili ni walimu ambao wamepandishwa madaraja hawajapewa madaraja yanayostahiki na hakuna vifaa vya kufundishia baada ya kufanyika kwa mabadiliko ya mtaala wa elimu.

Akifungua mkutano huo, Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego aliwaagiza wakurugenzi wa halmashauri na wakuu wa wilaya kutokalia madai ya watumishi muda mrefu badala yake wayafanyie kazi.





# Wakulima wa soya waanza kutumia chanjo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKULIMA wa soya katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini wameanza kutumia chanjo maalumu ya zao hilo, iliyofanyiwa utafiti kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Morocco.

Hali hiyo itaongeza tija kwenye uzalishaji wa zao hilo kwa zaidi ya asilimia 30.

Watafiti wa kilimo kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) Kituo cha Uyole kilichoko jijini Mbeya, wameanza kutoa elimu ya matumizi ya chanjo hiyo kwa wakulima, ili waitumie kwa usahihi na kuongeza tija.

Mtafiti wa udongo kutoka TARI Kituo cha Uyole, Fedrick Mlowe, alisema wanawafundisha wakulima wa zao hilo matumizi sahihi ya chanjo pamoja na matumizi ya mbolea ya kupandia ili kuongeza tija na kupunguza gharama za uzalishaji.

Alisema chanjo hiyo inaongeza tija kati ya asilimia 30 na 40 endapo mkulima ataitumia kwa usahihi na kuhudumia vizuri shamba lake pamoja na kufuata mbinu bora za kilimo.

Mlowe alisema mkulima akilima soya kwa kutumia mbolea ya kupandia pekee anaweza kupata gunia 10 mpaka 15 kwa ekari moja na endapo atatumia chanjo anaweza kuongeza uzalishaji kwa kupata kati ya gunia 15 na 20.

"Chanjo peke yake inamsaidia mkulima kuondokana na matumizi yasiyokuwa ya lazima ya mbolea ya kukuzia mpaka mifuko mitatu, kwa hiyo mkulima akitumia chanjo hii anaongeza tija na anapunguza gharama za uzalishaji," alisema Mlowe.

Alisema elimu ya matumizi ya chanjo hiyo wameshaitoa katika mikoa sita ya Nyanda za Juu Kusini ambayo ni Mbeya, Iringa, Ruvuma, Rukwa, Katavi na Songwe na kwamba wamekuwa wakitumia mashamba darasa kuwafundisha wakulima kwa vitendo.

Mkurugenzi wa TARI) Uyole, Dk. Dennis Tippe alisema mbali na chanjo hiyo kuongeza tija kwenye uzalishaji pia inasaidia kulinda afya ya udongo kwa kupunguza matumizi ya mbolea ambazo zinazalisha tindikali.

Alisema chanjo hiyo ikitumika vizuri inasaidia kuboresha mashamba na kusaidia kuongeza tija kwa zaidi ya msimu mmoja ambao mkulima anatumia shamba lake.

Alisema endapo mkulima atalima soya msimu wa kwanza kwa kutumia chanjo hiyo, anaweza kulima zao lingine msimu unaofuata kwenye shamba hilo hilo na akapata mavuno mazuri kutokana na mabaki ya chanjo.

Baadhi ya wakulima wa mikoa hiyo walioshiriki mafunzo ya matumizi ya chanjo, walisema itawasaidia kuondokana na kilimo cha mazoea ambacho kimekuwa na tija ndogo ikilinganishwa na kile wanachoambiwa kuwa wanastahili kupata.

Mmoja wa wakulima hao, Salanji Mataka kutoka katika Wilaya ya Namtumbo mkoani Ruvuma, alisema mafunzo hayo yatawasaidia kuongeza uzalishaji na kukidhi mahitaji ya soko la nje na ndani.

Alisema wamekuwa wakilima kwa kutumia mbinu za asili ambazo zimekuwa zikiwapatia matokeo kidogo na hivyo hata kipato kuwa cha kawaida.



Mtafiti wa Udongo kutoka TARI Kituo cha Uyole, Fedrick Mlowe (kushoto), akitoa elimu ya matumizi ya chanjo ya soya kwa baadhi ya wakulima wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini katika moja ya mashamba darasa yaliyopo Wilaya ya Namtumbo mkoani Ruvuma mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Watatu wafariki dunia ajali ya lori

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATU watatu wamefariki dunia na mmoja kujeruhiwa baada ya lori lililokuwa limebeba shehena ya makaa ya mawe kufeli breki, kuparamia watembea kwa miguu katika eneo la Uyole jijini Mbeya.

Lori hilo lenye namba za usajili T. 853 EDB lilipata ajali hiyo juzi ambapo linadaiwa kuwa lilikuwa likitokea katika mgodi wa makaa ya mawe wa Kiwira uliopo wilayani Ileje likielekea Songwe viwandani.

Mashuhuda wa ajali hiyo walisema ndani ya lori hilo walikuwamo watu watatu ambao ni dereva na msaidizi wake pamoja na mwanamke mmoja ambao wote walifariki eneo la tukio.

Mmoja wa mashuhuda wa tukio hilo, Kelvin Mwasaga, alisema lori hilo lilikuwa linatokea eneo la Maghorofani likiwa na mwendo mkali na lilipofika katika eneo hilo dereva alishindwa kulimudu na ndipo likapinduka na kujiburuza umbali wa zaidi ya mita 100.

Alisema kwenye eneo la tukio waliwakuta watu watatu ambao walikuwa kwenye gari na mmoja alikuwa mfanyabiashara mdogo ambaye alikuwa anauza nguo.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaaa wa Iwambala ilipotokea ajali hiyo, Zawadi Mwalyambi alisema baada ya kupata taarifa ya ajali alikwenda katika eneo la tukio.

Alisema baada ya kufika eneo la tukio alikuta mwili mmoja umeshatolewa nje lakini mingine ilikuwa inaonekana ndani ya gari na ilikuwa vigumu kuiondoa kutokana na gari hilo kuharibika.

Alisema askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji walifika eneo la tukio na kuanza uokoaji.

Alisema baada ya kuiinua lori hilo ndipo walifanikiwa kuiondoa miili miwili iliyokuwa imekwama na kuipeleka katika chumba cha kuhifadhia maiti Hospitali ya Igawilo.

Mkaguzi Msaidizi wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Mbeya, Columbus Boniface alisema walipata wito saa 5:15 kuwa kuna lori lilikuwa limepata ajali na hivyo wakaanza safari kuelekea eneo la tukio.

Alisema kazi ya kuondoa miili ilikuwa ngumu lakini kutokana na ushirikiano uliokuwepo walifanikiwa baada ya kuliinua gari hilo.

Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Mbeya, Mrakibu Mwandamizi wa Polisi, Hussein Gawile alisema eneo ilipotokea ajali hiyo limekuwa hatarishi kutokana na ajali nyingi kutokea mara kwa mara.

# Waomba elimu ya maendeleo kutolewa Mkongobaki

**Na Elizabeth John,** LUDEWA

WANANCHI wa vijiji vya Ugera na Lupangara Kata ya Mkongobaki Wilaya ya Ludewa mkoani Njombe, wameiomba serikali kutoa elimu ya maendeleo kwa baadhi ya wananchi waliokaidi kushiriki shughuli za maendeleo.

Walitoa ombi hilo juzi kwa Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, aliyefanya ziara ya ukaguzi kwenye Shule ya Sekondari Ugera.

"Hatutaki itumike nguvu ila wewe ni rais wa mkoa kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan, ndugu zetu wale hata wanafunzi tulisema waje hatuna ubinafsi lakini wamekataa," alisema Karoro Mtega.

Mwenyekiti wa kamati ya ujenzi wa shule hiyo, John Likwera, alisema shughuli za ujenzi wa shule hiyo zilifanywa na wananchi wa vijiji viwili pekee.

"Kulikuwa na changamoto katika usimamizi wa hii shule kwa maana Kijiji cha Kipagara na Ugera kwa hiyo nayo imekuwa bado shida kwa hiyo tunahitaji umoja kwa maana ya kata yetu Mkongobaki basi wote tufanye kazi lakini watoto wamepokelewa baadhi wanasoma," alisema Likwera.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Mtaka alisema jambo hilo amelichukua na anaandaa ziara ya kwenda kutembelea Kijiji cha Mkongobaki ili kuzungumza na wananchi wanaodaiwa kususia maendeleo.

Alisema: "Wazazi nawashukuru kwanza kwa kitendo cha kuamua kujitolea nguvu kazi kujenga shule hili ni jambo kubwa, nimepigiwa simu nyingi sana kuhusu shule hii kujengwa na wengine mmeingia kwenye mgogoro kwa sababu ya watoto wenu ambao hawapo hapa."

Naye Mkuu wa Wilaya ya Ludewa, Victoria Mwanziva, alisema watoto wa kata hiyo walikuwa wanapitia changamoto ya kupata elimu kwa sababu walikuwa wakitembea umbali mrefu zaidi ya kilometa 14.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ludewa, Sunday Deogratius, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa ajili ya kutoa fedha ili kujenga shule ya sekondari katika kata hiyo.





# ACT yaibua hoja miradi ya ujenzi Z'bar

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema miradi mingi ya ujenzi Zanzibar ina kasoro, hata kuibua hoja ya uadilifu wa wanaosimamia utekelezaji wake.

Kimesema baadhi ya miradi hiyo imetekelezwa pasi na idhini ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar, jambo ambalo kinalitaja ni kinyume na Sheria ya Zabuni Zanzibar.

Hayo yalisemwa jana na Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Ismail Jussa Ladhu, alipokuwa akizungumza katika mkutano wa ndani wa chama hicho, uliofanyika Kiembe Samaki, Mkoa wa Mjini Magharib Unguja.

Jussa alitoa mfano mradi wa ujenzi wa Jengo la Pili la Abiria Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume, ambalo linatarajiwa kutumia Dola za Marekani milioni 30 bila ya kuidhinishwa na Baraza la Wawakilishi katika bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024.

Aidha, alisema gharama za ukarabati Uwanja wa Amani, zimefikia Sh. bilioni 105 badala kutoka Sh. bilioni 56 matumizi ambayo pia hayakuidhinishwa na Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

Hata hivyo, alisema kwamba vitendo vya kasoro vitakoma mwaka 2025 baada ya ACT-Wazalendo kushika madaraka na kuhakikisha kinapambana na rushwa kwa vitendo.

Aidha, alisema pamoja na Bandari ya Malindi kubinafsishwa kwa wawekezaji kutoka Ufaransa bado huduma ni duni na kushuhudia tozo za huduma za bandari kuendelea kuongezeka na kuwaumiza wananchi wa Zanzibar.

Alisema Ripoti za Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali (CAG) zimekuwa zikifichua vitendo vya ubadhirifu na ufisadi unaofanyika katika taasisi za umma lakini hakuna watu wanaochukuliwa hatua na badala yake kuendelea kuwa tatizo sugu.

"Kwa mujibu wa ripoti ya CAG kuna wafanyakazi sita wamepewa mkopo wa Sh. bilioni moja na Benki ya Watu wa Zanzibar bila ya mkopo huo kuidhinishwa na bodi ya wakurugenzi wa benki hiyo jambo ambalo ni kinyume na sheria," alisema Jussa.

Naye Mwenyekiti wa chama hicho ambaye pia ni makamu wa kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman alisema, ACT hakina muda tena wa mazungumzo na serikali kuhusu mambo waliyokubaliana kabla ya kuungwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa na badala yake serikali inapaswa kutekeleza na siyo kufungua majadala wa mazungumzo.

Aidha, alisema kila mwananchi wa Zanzibar anahaki ya kuandikishwa na kuwa mpiga kura baada ya kupewa kitambulisho cha Mzazibari Mkaazi, cheti cha kuzaliwa na kuitaka serikali kuondosha urasimu katika vielelezo hivyo.

Akizungumzia mfumo wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, alisema kuna mambo yanafanyika Zanzibar ambayo yanakwenda kinyume na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1967.

Othman alisema kwa mujibu wa Katiba hiyo suala la Bandari, kodi ya forodha ni mambo ya muungano lakini mapato yamekuwa yakikusanywa na kubaki Zanzibar.

Alisema siku akatokea kiongozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na akaamua kusimamia mapato hayo kuingia katika Serikali ya Muungano, Zanzibar itakuwa na hali mbaya ya kiuchumi na kushindwa kulipa hata mishahara ya wafanyakazi kwa vile serikali inategemea mapato ya forodha na huduma za Bandari.

Alisema kwa msingi huo ACT kinaona ipo haja ya mfumo wa muungano kupitiwa upya ili Zanzibar kuwa na mamlaka kamili na kuondoa mambo yanayoleta migongano kikatiba katika utekelezaji wake ikiwamo suala la mafuta na gesi.




Makamu Mwenyekiti wa Chama cha ACT-Wazalendo, Ismail Jussa, akizungumza na viongozi wa chama hicho katika mkutano wa ndani uliofanyika Kiembe Samaki nje ya mji wa Zanzibar jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Serikali yataja sababu mfumo wa kodi kuwa rafiki

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Fedha na Mipango, imesema Serikali ya Zanzibar imechukua hatua za kutunga sera na sheria ambazo zinaendelea kuufanya mfumo wa kodi wa Zanzibar kuwa rafiki.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Juma Makungu, aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Mwanakwerekwe, Ameir Abdallah.

Ameir alitaka kujua kwa kiasi gani wafanyabiashara wa Zanzibar wanapata unafuu wa kodi kwa bidhaa wanazosafirisha kwenda Tanzania Bara.

Akijibu swali hilo, Makungu alisema serikali inafanya hayo ili kuweza kuimarisha mazingira mazuri ya uwekezaji yatakayowavutia wawekezaji wa ndani na nje na kufanya biashara ndani ya Zanzibar.

"Katika mwelekeo huo, wafanyabiashara wa Zanzibar ambao wanachukua bidhaa Zanzibar na kuzipeleka Tanzania Bara kwa lengo la kutafuta soko, wanapata unafuu wa kodi kwa mujibu wa sheria za kodi zilizopo," alisema.

Alisema wafanyabiashara hao wanapata unafuu wa kutolipa tena kodi waliyokuwa tayari wameshalipia Zanzibar na hutatakiwa kulipa tofauti ya kodi ya asilimia tatu katika Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa kodi ya ongezeko kwa sababu Tanzania Bara kiwango cha VAT ni asilimia 18.

Alisema ili mfanyabiashara aweze kunufaika na unafuu huo wa kutolipa kodi mara mbili ni lazima afuate taratibu za kuondosha mizigo Zanzibar na kupeleka Tanzania Bara kwa kuwa na nyaraka zote muhimu za kusafirisha mizigo hiyo zikiwamo nyaraka za kodi.

Alisema: "Mheshimiwa Spika kwa mara nyingine nitumie fursa hii kuwasisitiza wafanyabiashara wanaosafirisha mizigo kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara kufuata taratibu za kusafirisha mizigo na kuwa na nyaraka zote muhimu zinazotakiwa kwa mujibu wa sheria, ili kuondokana na usumbufu wa kulipa kodi mara mbili."

# Kiongozi wa Mwenge ahimiza matumizi nishati safi kupikia

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KIONGOZI wa Mbio za Mwenge kitaifa, Godfrey Mnzava, amesema umefika wakati wananchi kutumia majiko sanifu ili kupunguza uchafuzi wa mazingira.

Aliyasema hayo wakati akikabidhi majiko sanifu ya utumiaji wa nishati mbadala kwa wananchi wa Mwera Mkoa wa Mjini Magharib Unguja.

Alisema licha ya utumiaji wa nishati ya kuni kuharibu mazingira, pia umekuwa ukisababisha matatizo makubwa ya kimazingira kwa watumiaji wa nishati hiyo.

Alisema utumiaji wa nishati mbadala hauepukiki kwa sababu ndiyo chanzo cha kukinga mazingira na machafuko ya tabianchi.

Alisema kuwepo kwa mradi wa majiko sanifu inapunguza hasara na muda wa kuhangaikia ukataji wa kuni pamoja na uchomaji wa mkaa, hivyo ni vyema wananchi kutumia nishati mbadala kwa maendeleo ya jamii na serikali kwa ujumla.

"Ni vyema wananchi kuhamasika kutumia majiko sanifu ambayo yatalinda afya zao na jamii kwa ujumla,"alisema.

Mkuu wa Wilaya Magharibi 'A', Suzan Peter Kunambi, alisema shehia 31 kutoka Wilaya ya Magharibi A wamekabidhiwa majiko sanifu yanayotumia nishati mbadala ili kupunguza uharibifu wa mazingira.

Alisema Wilaya ya Magharibi inahamasisha jamii kuhusu matumizi sahihi ya nishati mbadala ili kutunza mazingira ya watu na viumbe hai.

Akitoa taarifa kuhusu majiko hayo, Tatu Hassan Abdalla kutoka Manispaa ya Magharibi A alisema nishati hiyo imeshafanyiwa utafiti na haina madhara kwa watumiaji.

Alisema katika kufikia malengo lazima jamii kuwa kitu kimoja kuelimishana juu ya utumiaji wa nishati mbadala kwa maendeleo ya taifa.

Majiko hayo 100 yamekabidhiwa kwa kina mamalishe na babalishe wa wilaya hiyo na yamegharimu zaidi ya Sh. milioni 1.9.

MIAKA 28 AJALI MV BUKOBA...

# Asimulia alivyopoteza mama na mdogo wake

**Na Christina Mwakangale**



NI miaka 28 tangu ajali ya meli ya Mv Bukoba ilipotea katika Ziwa Victoria, nchini. Zaidi ya watu 800 walipoteza maisha.

Iliweka rekodi ya dunia kuwa miongoni mwa ajali za chombo cha usafiri wa majini kusababisha vifo vya abiria wengi kwa wakati mmoja.

Inalinganishwa na ajali ya meli ya Titanic iliyotokea takribani miaka 100 iliyopita, ikisababisha vifo vya watu waliokadiriwa kufikia 2,000. MV Bukoba ilizinduliwa mwaka 1979 na Rais wa kwanza wa Tanzania, Julius Nyerere. Iliduмu kwa miaka 17 tu, ikiwa katika safari zake za kawaida, ikitokea katika Bandari ya Bukoba kupitia Kemondo.

Mei 21, mwaka 1996, siku kama ya leo, ni ukumbusho mbaya kwa Godwin Shinyanga, akifikiri kwamba pengine tukio hilo, limetokea jana.

"Bado kumbukumbu hazijafutika kichwani mwangu, bado nimebakiwa na maumivu makubwa," anakumbuka Shinyanga, wakati wa mahojiano yake maalumu na chombo cha habari TRT Afrika.

Shinyanga ni mtumishi wa umma, alimpoteza mama yake, Ritha Justus na mdogo wake aliyemfuata Evelyine, wakati akiwa na umri wa miaka sita tu, ajali ilitokea. Anasema kumbukumbu inakuwa mbaya zaidi kutokana na kushindwa kuwazika nduguze. Hadi leo, miili ya wapendwa wake haijawahi kupatikana. Utafutaji wa miili ulichukua siku tatu ndani ya maji kwenye ziwa hilo, ambalo ni kubwa barani Afrika.

Kwa mujibu wa Wikipedia, lina eneo la kilomita za mraba zaidi ya 68,100. Na kuwa ziwa kubwa kuliko yote barani Afrika na la pili duniani. Shinyanga, anasema familia yake ilizika magome mawili ya miti ziwani, kama ishara ya kuwakumbuka wapendwa wao.

Anafafanua kwamba, labda na yeye angekuwa ni sehemu ya waathirika wa ajali hiyo, ambayo iliua zaidi ya watu 800.

Wakati huo, Rais wa awamu ya nne, Benjamin Mkapa, alitangaza siku tatu za maombolezo. Watumishi wa serikali walichukuliwa hatua, kufuatia tukio hilo.

Shinyanga anasema kuwa wakati ajali inaotokea alikuwa anasoma kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Magu, mkoani Mwanza. Yeye pamoja na wanakwaya 32, walipanga safari ya kwenda Bukoba, kwa ziara ya Uinjilishaji, Mei 20, 1996.

"Nilikuwa ninaimba sauti ya tatu na nilikuwa ninapiga gitaa kwenye kwaya ya Imani kutoka Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), ambayo pia marehemu mama yangu alikuwa anaimbia," anasema Shinyanga.

Licha ya kufanya mazoezi ya mwisho pamoja na kwaya hiyo, Shinyanga hakuweza kuwa sehemu ya safari hiyo ya uinjilishaji.

"Waliondoka siku ya Jumatano na walifanikiwa kufika salama Bukoba na kufanya huduma ya uimbaji," anasimulia na kubainisha safari yao ya kurudi Mwanza ilianza jioni ya Mei 20, 1996.

Shinyanga anasema kuwa taarifa za kuzama kwa meli ya Mv Bukoba zilianza kuenea kwa kasi shuleni Magu, hali iliyoamsha wasiwasi mkubwa ndani ya moyo wake.

"Niliwasikia wanafunzi wenzangu wakisema kuwa kuna ajali kubwa imetokea Ziwa Victoria, hofu kubwa ilinijaa moyoni mwangu kwani ilikuwa ndio siku yao ya kurudi," anasema.

Hofu ilimjaa Shinyanga, ambaye alikuwa na miaka 16 wakati huo. Gari lilifika kumfuata shuleni kwao. "Nilihisi ubaridi mwilini mwangu, nikajua lazima kuna taarifa mbaya nitakazosikia."

### AJALI YENYEWE

Meli ya Mv Bukoba, ikiwa na abiria kati ya 750 na 800 pamoja na wafanyakazi 37, ilizama Ziwa Victoria mwambao wa Bwiru, jijini Mwanza, takribani kilomita 30 kabla ya kufika nchi kavu.

Tukio hilo,lilitokea asubuhi wakati wengi wa abiria wakiwa wanajiandaa kusafisha vinywa vyao.

Kulingana na simulizi za baadhi ya wanakwaya walionusurika kwenye ajali hiyo, mama mzazi wa Shinyanga, aliamua kubaki na Evelyine sehemu ya chini ya meli kutokana na hali ya baridi na upepo mkali kutoka ziwani.

"Wengi wao waliamua kupanda upande wa juu ya meli kwenda kupiga mswaki na kufurahia mandhari nzuri ya Jiji la Mwanza iliyoanza kuonekana asubuhi hiyo, kabla meli haijaanza kuyumba na hatimaye kuzama," anaeleza.

Mwaka huu, Shinyanga amepanga kwenda kufanya ibada katika eneo la Igoma, ambako kumejengwa mnara maalum wenye majina ya wale wote walipoteza maisha katika ajali hiyo.

"Jina la mama yangu na la mdogo wangu yako pale, itakuwa siku muhimu na ya tafakari kubwa sana katika maisha yangu," anasema.

Mwanamitindo Flaviana Matata pia alipompoteza mama yake kwenye ajali ya Mv Bukoba. Imekuwa ni desturi yake kila mwaka kutembelea makaburi ya waathirika yaliyoko katika eneo la Kitangiri, jijini Mwanza.


**TANGAZO KWA UMMA**
**KUZUIA MALI ZA MIRATHI**

Familia ya Lwakatare inapenda kuutaarifu Umma kwamba, kuanzia leo tarehe 21-5-2024 hakuna mmiliki aliyeidhinishwa na Mahakama kuuza au kufanya chochote juu ya mali zilizoachwa na Marehemu **GEORGE MUBEZI LWAKATARE** aliyefariki tarehe 12-02-2021.

Mali zote za Marehemu HAZIUZWI zikiwemo;

1. **Plot No. 438, Block J, Mbezi Beach, Dar es Salaam.**
2. **Plot No. 439, Block J, Mbezi Beach, Dar es Salaam.**
3. **Plot No. 589, Block J, Mbezi Beach, Dar es Salaam.**
4. **Plot No. 306, Block D, Mbezi Beach, Dar es Salaam.**
5. **Plot No. 186, Block B, Mbezi Beach, Dar es Salaam.**
6. **Plot No. 972, Block J, Mbezi Beach, Dar es Salaam.**
7. **Plot No. 260, Block E, Tegeta, Dar es Salaam.**
8. **Plot No. 262, Block E, Tegeta, Dar es Salaa.**
9. **Plot No.45, Block B, Kisesa, Mwanza.**
10. **Plot No. 467, Block Y, Ngarenaro, Arusha.**
11. **Plot No. 301, Kijitonyama, Dar es Salaam.**
12. **Plot No. 302, Kijitonyama, Dar es Salaam.**
13. **Plot in Salasala, Dar es Salaam 3 ½ Hectares.**
14. **Plot No. 79, Block M, Kilwa Masoko.**
15. **Plot No.13, Block J, Mwangaza, Dodoma.**
16. **A plot in Mbweni JKT, Kinondoni, Dar es Salaam.**

Namba ya Mirathi ni Na. 65 ya 2021 na Na. 2834 ya 2024.
Watu wote wanaelezwa kuwa Mali zote za Marehemu zilizo orodheshwa hapo juu haziuzwi, kwani bado hakuna mmiliki wa mali za marehemu kwasasa mpaka pale Mahakama itakapotoa tamko la mwisho.

***Tangazo hili limetolewa na familia ya Lwakatare***



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Wilaya ya DODOMA**

**Kituo cha MJINI Mkoa DODOMA**

**Usimamizi wa mirathi Na 31/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU MAYANI MAULIDI WAZIRI KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA CHIKU HAMIS SIZYA**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 24 Mwezi 5 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

- Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani na waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika

Imetolewa leo Tarehe 17 Mwezi 05 Mwaka 2024



**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT**
**CAP 117**
**CHANGE OF NAME BY DEED POLL**

**I,EZILEY GODBLESS KWAYU,** a male ,Tanzanian,an adult,Christian and resident of Njiapanda Ward,in Moshi District,Kilimanjaro Region ,Tanzania,formerly known as **PATRIC GODBLESS KWAY** do hereby absolutely renounce and abandon the use of my former name of **PATRIC GODBLESS KWAY** which appears in my citizen identity card with number **(19971228252320000120)** which has not been printed out,and in lieu thereof do assume and adopt the name of **EZILEY GODBLESS KWAYU,** which appears in my certificate of secondary education with number (S.1022-0255)
Pursuant to such change of name as aforesaid **I DECLARE THAT** I shall at all times hereinafter in all Records ,Deeds and Instructions in writing and in all actions and proceedings and in all dealings and transactions and upon all accessions whatsoever use and assign the said name of **EZILEY GODBLESS KWAYU** as my name in lieu of the said **PATRIC GODBLESS KWAY**
**AND I HEREBY, BY THIS DEED, AUTHORISE AND REQUEST** all persons to designate and address me in the name of **EZILEY GODBLESS KWAYU** , and in the manner hereinafter appearing .
**I DO FUTHER DECLARE THAT** all deeds, documents, transactions,dealings, records and any other instruments in which my former name **PATRIC GODBLESS KWAY** appear are valid.

SIGNED AND DELIVERED at Moshi Municipality by the said Eziley Godbless Kwayu who is known to me personally/identified to me by ............ the Latter being known to me personally, in my presence on this ...24th day of June. 2022 — DEPONENT

BEFORE ME:
Name: ...
Address: P.O. Box 1446 Moshi
Qualification: ADVOCATE
Signature: ...
Date: 24th JUNE 2022



**KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI**

**HALIMA ALPHONCE BANDA** anatangaza kupotea kwa kadi za pikipiki zenye usajili namba **MC 419 AYZ, MC 558 CUT na MC 569 CYB.** Kwa yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:
**PHQ/TAN/TAN/4792/2024**



**KUPOTEA KWA VYETI**



**AMIR HAMUD** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0455-0038 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia TWEYAMBE SECONDARY SCHOOL mwaka 2002 na cheti cha kidato cha sita chenye index namba S0137-0767 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia MKWAWA HIGH SCHOOL mwaka 2005. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: PHQ/SAR/ILA/11585/2023**



**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**

**DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO.10341 OF 2024**

**In the Matter of the Etate of the late MARIA JACKSON MANDWEKE**

**By 1.LUCIA JACKSON MANDWEKE**
**2..........................................**

ALL persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above- named pepetitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 23 day of MAY 2023.

Dated at Morogoro this 15 day of MAY 2024.

RESIDENT MAGISTRATE



**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**MASUDI MAHAMOUD MSANGI** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA **TOYOTA NOAH,** RANGI NYEUPE YENYE USAJILI **T966 DBB** KWA YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE

POLISI TAARIFA
**PHQ/IRI/IRI/6816/2024.**



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA**

**FORM II**

**SMM 1994 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya Mwanzo ya Mwambao wilaya ya Bagamoyo, Mkoa wa Pwani. Ombi la ndugu **RAMADHANI SALEHE ABDALLAH** kuteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi namba 28/2024 ya marehemu **ALLY MWINYIMKUU KIDUGA** Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na marehemu huyo wanaalikwa kuja kuhudhuria kesi hii wakitaka mnamo tarehe 11/06/2024 kabla huyu mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hii.
Wasia wa Marehemu

SAHIHI YA HAKIMU

TAREHE: 16/05/2024



**KUPOTEA KWA CHETI**



**TUMAINI DAUD PHILIPO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1239/0281/2007** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia shule ya sekondari SAMUYE mwaka 2007. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha polisi. POLISI TAARIFA: **MWA/NY/RB/371658/2019**



**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**IN THE DISTRICT COURT OF ARUSHA**
**AT ARUSHA**

**CIVIL CASE NO. 1396 OF 2024**

**BANK OF AFRICA TANZANIA LIMITED PLAINTIFF**

**VERSUS**

**SMAFFLE SAMSON JADWA DEFENDANT**

**NOTICE OF MENTION**

**TO SMAFFLE SAMSON JADWA**

**TAKE NOTICE** that the above has been fixed for mention in the District Magistrate's court of Arusha on the 24 May 2024 at 9: 00 O'clock in the afternoon
You may appeal in person or by Advocate or agent duly authorized to appeal on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.
**TAKE FURTHER NOTICE** that in default of your appearance on that day time before mention or hearing the court may proceed in your absence.
**GIVEN** under my hand and the seal of the court this 16 day of MAY/2024

RESIDENT MAGISTRATE

# Mokhber kuongoza siku 50 baada ya Rais Iran kufariki

Na Maulid Mmbaga

KIONGOZI wa juu wa Iran, Ayatollah Khamenei, mwenye kauli ya mwisho katika masuala yote ya kitaifa, amemteua Makamu wa Kwanza wa Rais wa nchi hiyo, Mohammad Mokhber, kukaimu nafasi ya urais baada ya Rais wa taifa hilo, Ebrahim Raisi, kufariki katika ajali ya helikopta.

Kwa mujibu wa katiba ya Iran, makamu wa kwanza wa rais anastahili kuchukua wadhifa huo iwapo rais atafariki, kuondolewa madarakani, kujiuzulu au kuwa mgonjwa kwa kipindi cha zaidi ya miezi miwili. Huku ikielezwa kuwa Mokhber atakaimu nafasi hiyo kwa siku 50 kabla ya kufanyika kwa uchaguzi.

Televisheni ya taifa IRNAA ilisema ajali hiyo ilitokea Jumapili karibu na eneo la Jolfa, kilomita 600 kutoka Tehran karibu na mpaka wa Azerbaijan, ikielezwa kuwa chanzo cha ajali hiyo ni hali mbaya ya hewa iliyosababisha helikopta hiyo kupotea kwenye rada.

Ilibainishwa kuwa hali mbaya ya hewa pia ilitatiza shughuli za utafutaji huku rais akiwa ametoweka kwa zaidi ya saa 12 hadi mapema jana tangu kutokea kwa ajali hiyo, juzi.

Pia ilielezwa kuwa ndani ya helikopta hiyo kulikuwa na viongozo kadhaa walioongozana na Rais Raisi, akiwamo Waziri wa Mambo ya Nje Hossein Abdollahian, Ayatollah Mohammad, imamu wa Swala ya Ijumaa katika mji wa Tabriz na Jenerali Malek Rahmati, gavana wa jimbo la Azabajani Mashariki.

Wengine ni kamanda wa kitengo cha ulinzi wa rais, Sardar Mousavi, pamoja na walinzi kadhaa na wafanyakazi wa helikopta ambao bado hawajatajwa, huku ikielezwa kuwa hapakuwa na mtu aliyenusurika katika eneo la ajali.

Ilielezwa kuwa Rais Raisi ambaye amekutwa na umauti akiwa na umri wa miaka 64 na wasaidizi wake walikuwa wakisafiri kurudi nyumbani wakitoka kwenye mkutano na Rais wa Azerbaijan Ilham Aliyev.

"Baada ya timu ya waokoaji kufika eneo la ajali walipata mabaki ya helikopta hiyo na hapakuwa na dalili zozote za abiria wa helikopta hiyo kuwa hai hadi sasa," ilisema taarifa hiyo.

Mkuu wa Shirika la Hilali Nyekundu la Iran, Pirhossein Koolivand, alisema timu za uokoaji zilikuwa zikiendelea kusogea karibu na eneo la ajali licha ya hali hewa kuwa mbaya.

Nchi kadhaa zikiwamo Russia na Uturuki zilitoa msaada katika operesheni ya uokoaji, na kwamba ndege isiyo na rubani ya Uturuki pia iliruka katika anga ya Iran kusaidia shughuli ya utafutaji. Huku Kiongozi wa juu wa Iran Ayatollah Ali Khamenei ambaye ndiye aliye na mamlaka makubwa kuhusiana na masuala yote ya kitaifa, akitoa wito kwa Wairan kumwombea Rais Raisi.



Rais wa Iran, Ebrahim Raisi aliyefariki katika ajali ya helikopta juzi. **PICHA ZOTE: MTANDAO**



Makamu wa Kwanza wa Rais wa Iran, Mohammad Mokhber, aliyeteuliwa kushika nafasi ya urais kwa siku 50.

> Rais Raisi, ambaye alifariki katika ajali, alikuwa akikaribia mwisho wa muhula wake wa kwanza wa kipindi cha miaka minne kama rais.

**MATAIFA YAOMBOLEZA**

Nchi mbalimbali duniani na viongozi wake wameendelea kuomboleza kwa kutuma salama za pole kwa raia wa Iran baada ya kumpoteza Rais Raisi.

Waziri Mkuu wa Pakistan, Shehbaz Sharif, alitangaza siku ya maombolezo ya kitaifa ambako bendera zote zitapeperushwa nusu mlingoti kumuenzi kiongozi huyo wa Iran.

Kiongozi huyo wa Pakistani alikuwa mwenyeji wa Rais Raisi mjini Islamabad kwa ziara ya siku tatu mwezi Aprili katika ziara ya kujaribu kuboresha uhusiano kati ya mataifa hayo jirani kufuatia mashambulio ya kila upande mapema mwaka huu.

Umoja wa Ulaya nao pia umeeleza kusikitishwa na kifo cha Rais Raisi. Huku Waziri wa Mambo ya Nje wa Russia, Sergei Lavrov katika taarifa yake, akisema kiongozi huyo na waziri wake wa mambo ya kigeni Amir-Abdollahian walikuwa marafiki wa Russia.

Naye Rais Vladmir Putin alimtaja Rais Raisi kama kiongozi mwenye utofauti. Huku Rais Bashar al- Assada wa Syria kwa akionyesha kusimama pamoja na raia wa Jamhuri ya Iran kutokana na kifo cha kiongozi wao.

Wizara ya Mambo ya Kigeni ya China kupitia taarifa yake, ilisema Rais Xi Jinping ameelezea kifo cha Raisi kama pigo kubwa kwa raia wa Iran.

Nao wapiganaji wa Hamas wamemtaja kiongozi huyo kama mtu aliyewaunga mkono kwa dhati wapiganaji hao wanaoungwa mkono na Tehran. Huku wapiganaji wa Hezbollah wanaoungwa mkono pia na Iran, wakimtaja kama mtetezi wa makundi yanayoipinga Israel.

**HISTORIA YAKE**

Rais Raisi aliapishwa kama rais mpya wa Iran Agosti 2021, baada ya kushinda uchaguzi wa urais Juni kwa chini ya asilimia 62 ya kura kama mgombea mkuu wa vyama vya siasa kali na anayependwa zaidi.

Ilielezwa kuwa mara ya mwisho, wapinzani wote wakubwa kwa Raisi walizuiwa kugombea, hivyo kumsafishia njia ya kuingia ofisini akiwa na idadi ndogo zaidi ya wapigakura takriban asilimia 30 ya wapigakura wanaostahiki, huku wengi wakisusia walichokiona kama uchaguzi maalum.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa Raisi alizaliwa 1960 huko Mashhad, kaskazini mashariki mwa Iran, ikielezwa kwamba anazingatiwa kuwa na ushawishi mkubwa ndani ya mfumo wa Jamhuri ya Kiislamu, kwa kudumisha uhusiano wa karibu na Khamenei.

Kwa mujibu wa katiba, Raisi alikuwa ni kiongozi namba mbili nchini Iran, akimfuata Khamenei aliye mkuu wa nchi na pia ndiye mwenye uamuzi wa mwisho katika masuala yote ya kimkakati.

Vile vile, ilielezwa kuwa hatima mbaya ya rais wa Iran mwenye misimamo mikali haitarajiwi kuvuruga mwelekeo wa sera ya Iran au kuitikisa Jamhuri ya Kiislamu kwa njia yoyote ile.

Rais Raisi, ambaye alifariki katika ajali, alikuwa akikaribia mwisho wa muhula wake wa kwanza wa kipindi cha miaka minne kama rais.

Ilibainishwa kuwa uchaguzi utafanyika baada ya siku 50 kumchagua rais mwengine kwa mujibu wa katiba ya nchi hiyo. Na kwamba jopo linalojumuisha spika wa bunge, rais wa mahakama na makamu wa rais wamepewa majukumu ya kupanga uchaguzi mkuu wa kitaifa.

Mokhber (68), aliteuliwa kuwa makamu wa Rais Raisi alipochukua wadhifa huo Agosti 2021 na kwamba alizaliwa katika mji wa Dezful, Kusini Magharibi mwa jimbo la Khuzestan, ambako alihudumu katika nafasi tofauti za serikali. **Chanzo mashirika ya kimataifa**

# GAMONDI AIVULIA KOFIA IHEFU FC

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Kocha Mkuu wa Yanga, Muargentina, Miguel Gamondi, akiwapongeza Ihefu FC kwa kucheza kwa kiwango cha juu na kuwapa wakati mgumu kwa dakika zote 120 za nusu fainali ya Kombe la FA lililochezwa juzi, Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, jijini Arusha, Kocha Mecky Maxime, amesema hana cha kuwadai wachezaji wake kwani walipambana vya kutosha.

**Wakizungumza kwa nyakati tofauti baada ya kumalizika kwa mechi hiyo ambayo Yanga ilishinda bao 1-0, makocha hao kila mmoja alitoa maoni kutokana na mchezo huo.**

Gamondi alikiri kuwa hali ilikuwa ngumu, wapinzani wao walitengeneza nafasi tatu za wazi dakika 90 za mchezo ambazo zingeweza kuamua matokeo ya mechi, lakini hawakuzitumia vyema.

"Ilikuwa mechi ngumu, wapinzani wetu walitengeneza nafasi tatu za wazi ambazo wangeweza kutuadhibu na tukaikosa fainali, tulitawala mechi kipindi cha pili, ila mabeki wa Ihefu walizuia vizuri sana," alisema kocha huyo.

Alibainisha kuwa utimamu wa mwili na pumzi waliokuwa nao wachezaji wao ndiyo, uliowafanya kuibuka na ushindi.




"Dakika 30 za nyongeza tulizotumia ni utimamu wa mwili wa wachezaji wangu ndiyo ulioamua mechi, tukashinda, nawapongeza Ihefu wamecheza vizuri sana, walipambana, wachezaji wake ni wapambanaji," alisema Gamondi.

Kwa upande wake, Maxime, alisema anasikitika kwa sababu wametolewa, lakini kwa jinsi walivyocheza wachezaji wake, hana cha kuwadai.

"Tunasikitika kwa sababu tumetoka, lakini mechi ilikuwa nzuri kwetu, tulipambana kadri ya uwezo wetu, nafikiri mechi ilikuwa ya kiufundi zaidi, ni makosa machache tu yaliyotokea ndiyo wameweza kutuadhibu, bao moja limeamua matokeo. Nawapongeza wachezaji wamecheza vizuri, sina cha kuwadai," alisema Maxime.

Ushindi huo wa Yanga unawafanya kutinga hatua ya fainali ambapo sasa itacheza dhidi ya Azam FC Juni 2, Uwanja wa Tanzanite mkoani Manyara.




Timu ya wasichana wenye umri chini ya miaka 16 ya Bulls Football Academy wakishangilia ubingwa wa michuano ya vijana ya 'Dar Youth Cup Min' jijini Dar es Salaam juzi baada ya kuzishinda timu nyingine 28 za wasichana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Kocha Hilali: Tunautaka ubingwa Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA wa klabu ya Zimamoto FC Mohamed Hilali, amesema kutokana na uwezo mkubwa unaoonyeshwa na wachezaji wake kwenye michezo ya Ligi Kuu Zanzibar, ana uhakika wa kuchukua ubingwa msimu huu.

Zimamoto SC inashika nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi hiyo wakiwa na pointi 49 baada ya kucheza michezo 24 mpaka sasa.

Juzi timu hiyo ilifanikiwa kuibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Jamhuri na kufikisha idadi hiyo ya pointi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Hilali alisema michezo sita iliyobakia atahakikisha anafanya vizuri ili kutimiza ndoto yake ya kuchukua ubingwa.

Alisema kutokana na kiwango cha wachezaji wake kuzidi kuimarika katika kila mchezo inampa matumaini na nguvu katika kuweka juhudi zaidi ili kufanikisha lengo lao.

Alisema ingawa ushindani ni mkubwa kwa timu nne za juu hilo halipotezi matumaini yake ya kutwaa taji la Ligi Kuu msimu huu.

"Kila mchezo tunaocheza kikosi chetu kinazidi kuimarika zaidi katika mbio za ubingwa, kwa sasa hatuwaangalia wenzetu wapo wapi tunachoangalia timu yetu tunataka nini," alisema.

Aidha alisema kuwa mpaka sasa wachezaji wake wote katika kikosi hicho wapo makini na wanacheza kwa tahadhari kuepuka majeraha.

Timu hiyo Mei 23 itashuka uwanjani tena kuumana na Kipanga FC.

JKU wanaongoza msimamo wa Ligi Kuu ya Zanzibar wakiwa na pointi 53, nafasi ya tatu inashikiliwa na bingwa mtetezi wa ligi hiyo, KMKM wenye pointi 48.

## Sita kuchuana Simiyu

**Na Somoe Ng'itu**

WAGOMBEA sita wamepitishwa kuwania nafasi mbalimbali katika uchaguzi wa Chama cha Mpira wa Miguu cha Wanawake Mkoa wa Simiyu (SWFA), utakaofanyika Ijumaa, imefahamika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi, Gloria Ikanda, aliwataja waliopitishwa kuwania nafasi ya uenyekiti kuwa ni Rehema Shalali na Devotha Soko.

Ikanda aliwataja wanaochuana katika nafasi ya Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa TWFA ni Masela Owenya na Rose Zacharia wakati wanaowania nafasi ya Ujumbe wa Kamati ya Utendaji ni Rebecca Silinde na Asha Mussa.

"Tunapenda kuwakumbusha wagombea wote kufuata kanuni na taratibu za uchaguzi huu, tunaamini pia watafanya kampeni za busara na si vinginevyo," alisema Ikanda.

Wakati huo huo, Chama cha Mpira wa Miguu cha Wanawake Mkoa wa Tanga (TRWFA), kimepanga kufanya uchaguzi wake Juni 2, mwaka huu.

## *Hatima Copco, Warriors kubaki, kushuka 'Championship' leo*

**Na Adam Fungamwango**

HATIMA ya timu za Copco na Green Warriors kubaki au kushuka daraja kwenye Ligi ya Championship inatarajiwa kujulikana leo wakati zitakapocheza mechi zao za 'play off' dhidi ya Mwadui na Malimao FC za daraja la pili 'First League.'

Copco, itakuwa kwenye uwanja wake wa nyumbani, Nyamagana kucheza dhidi ya Mwadui FC, huku maafande wa Green Warriors wao watakuwa, Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, Dar es Salaam, kucheza dhidi ya Malimao FC kutoka Katavi.

Hata hivyo, Copco itakuwa na kibarua kigumu cha kubaki Ligi ya Championship kwani itabidi ipate ushindi wa angalau mabao 4-0 kutokana na kukubali kipigo cha mabao 3-0 kwenye mchezo wa kwanza uliochezwa, Uwanja wa Nyankumbu, Geita.

Iwapo Mwadui itafanikiwa kulinda ushindi wake, itapanda daraja kutoka 'First League' na kuishusha Copco FC.

Hali si nzuri kwa Green Warriors, kwani katika mechi ya kwanza ya 'play off', iliyochezwa Mei 17, Uwanja wa Kituo cha Michezo cha TFF kilichopo Kigamboni, ilishinda mabao 2-0, hivyo itahitaji kuulinda ushindi huo ili isalie Championship na kuiacha Malimao kubaki 'First League'.

Warriors kama wataruhusu kupoteza mchezo huo kwa zaidi ya mabao 3-0 watashuka daraja.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### KUPUNGUZIWA MSHAHARA

KLABU ya Manchester United wanataka takriban asilimia 75 ya pauni milioni 75 walizolipa Borussia Dortmund kwa winga wa Uingereza, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 24, ambaye atahitaji kupunguzwa mshahara wake wa pauni 275,000 kwa wiki ikiwa klabu hiyo ya Bundesliga itakamilisha dili la kumsaini tena. ***(Sun)***

### SESKO AONGEZEWA

RB Leipzig wamempa mshambuliaji wa Slovenia, Benjamin Sesko mwenye umri wa miaka 20 nyongeza ya mkataba wa mwaka mmoja, nyota huyo alikuwa akinyemelewa na Arsenal. ***(Fabrizio Romano)***

### SOUZA ANGEIGHARIMU

KLABU ya Sheffield United ingelazimika kulipa kiasi cha tarakimu sita kwa kiungo wa kati wa Brazil, Vinicius Souza kwa klabu yake ya zamani ya Lommel iwapo mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 angeanza katika mechi dhidi ya Tottenham Hotspur Jumapili. ***(Sun)***

### HAG AGOMBEWA ULAYA

BEYERN Munich na Ajax wanaendelea kupigania sahihi ya Erik ten Hag mwenye miaka 54, kwa imani kwamba atafutwa kazi kama kocha wa Manchester United mwishoni mwa msimu huu. ***(Mirror)***

### RAYA, ARSENAL BADO

KIPA wa Hispania, David Raya mwenye umri wa miaka 28 amesema hajafanya mazungumzo yoyote na Arsenal kuhusu iwapo watafanya uhamisho wake wa mkopo kutoka Brentford kuwa wa kudumu. ***(Express)***

### ANGE KUSAJILI STRAIKA

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Ange Postecoglou, ataweka kipaumbele kumsajili mshambuliaji mpya na kiungo wa safu ya ulinzi huku akipanga kuwaachilia wachezaji wengi msimu wa joto. ***(Mirror)***

### MCKENNA KUBAKIZWA

KLABU ya Iswich inasema wanafanya kila linalowezekana kusalia na kocha Kieran McKenna huku klabu za Brighton, Chelsea na Manchester United zikiwa na mpango wa kumchukua. ***(Teamtalk)***

### POCHETTINO NA KIKOSI

KOCHA Mauricio Pochettino amesema atafurahi kusalia na asilimia 80 hadi 85 ya kikosi chake msimu ujao.***(football.london)***

### ARSENAL YATAKA UBINGWA

MWENYEKITI mwenza wa Arsenal, Josh Kroenke amewaambia mashabiki "klabu haitasimama tuli" inapotafuta wachezaji ili kusaidia kupata taji la England na Ulaya. ***(Goal)***

### BROWN KUTUA W'HAM

KLABU ya West Ham wanakaribia kumsajili mlinzi mwenye umri wa miaka 18 raia wa Uingereza, Luis Brown kutoka Arsenal. ***(Caught Offside)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# HAALAND ASHINDA KIATU CHA DHAHABU

**LONDON,** England

ERLING Haaland alishinda Kiatu cha Dhahabu cha Ligi Kuu England kwa msimu wa pili mfululizo baada ya kufikisha mabao 27 huku timu yake Manchester City ikitwaa taji.

**City walitwaa taji lao la nne mfululizo la Ligi Jumapili baada ya kuifunga West Ham 3-1 kwenye Uwanja wa Etihad na kumaliza pointi mbili mbele ya Arsenal, ambao walishinda mchezo wao wa mwisho msimu huu dhidi ya Everton.**

**Tuzo hiyo ni ya pili mfululizo kwake baada ya kufanya hivyo msimu uliopita...**

Hata hivyo Halaand ameshindwa kurudia mafanikio yake ya msimu uliopita katika upachikaji mabao alipofunga jumla ya mabao 36 kwenye ligi, mabao yake 27 msimu huu yalimfanya kumpiku Cole Palmer wa Chelsea mwenye miaka 22.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Norway amekosolewa kwa uchezaji wake msimu huu, haswa na nahodha wa zamani wa Manchester United, Roy Keane ambaye alimwita "Mchezaji wa Ligi ya Pili" baada ya sare tasa ya City dhidi ya Arsenal mwezi Aprili.

Kujibu maoni ya Keane, bosi wa City Pep Guardiola alimsifu Haaland kama "mshambulaji bora zaidi duniani."

# USYK AMCHAPA FURY NA KUWA BINGWA WA DUNIA



**RIYADH,** Saudi Arabia

BONDIA Tyson Fury alipigwa kwa pointi nchini Saudi Arabia na Oleksandr Usyk ambaye sasa ni bingwa wa kwanza wa ndondi za uzito wa juu duniani kushikilia mikanda minne.

Katika usiku huo wa juzi uliosheheni ujuzi wa kila aina kutoka kwa mabondia hao, Fury alianza vyema mechi hiyo lakini akaokolewa na kengele katika raundi ya tisa kutokana na kichapo kutoka kwa Usyk.

Akiwa katika hali ya kusubiri matokeo kusomwa, Fury alionekana kushawishika kupata ushindi kabla ya Usyk kutangazwa mshindi.

Matokeo hayo yalisomeka 115-112 na 114-113 kwa raia huyo wa Ukraine huku jaji wa tatu akitoa pointi 114-113 kwa Fury.

Hii ilimaanisha Fury mwenye miaka 35, alipoteza kwa mara ya kwanza katika kipindi cha miaka 16.

Atapata fursa ya kulipiza kisasi kwa mechi ya marudiano iliyopangwa kufanyika baadaye mwaka huu.

"Ninaamini alishinda raundi chache, lakini nilishinda nyingi," alisema Fury baada ya pambano hilo.

"Ilikuwa moja ya maamuzi mabaya zaidi katika historia ya ndondi. Nitarejea."

Usyk anachukua mkanda wa WBC kutoka kwa Fury, ili kuongeza kwenye mkusanyiko mikanda yake ya WBA, WBO na IBF.

Bondia huyo mwenye miaka 37 bado hajapigwa na anakuwa bondia wa kwanza katika takriban miaka 25 kusimama kidete kama bingwa pekee wa dunia wa uzito wa juu.

# Guardiola adokeza kuondoka City

**MANCHESTER,** England



PEP Guardiola amedokeza kuwa msimu ujao unaweza kuwa wa mwisho kwake kama kocha wa Manchester City.

Guardiola aliiongoza timu yake kutwaa taji la nne mfululizo la Ligi Kuu England kwa ushindi wa 3-1 dhidi ya West Ham kwenye Uwanja wa Etihad juzi Jumapili.

Mhispania huyo ana mkataba hadi 2025 ambao ananuia kuuheshimu, lakini kocha huyo mwenye miaka 53 alisema huenda hasisaini mkataba mwingine mpya.

"Ukweli ni kwamba ninakaribia kuondoka kuliko kubaki," alisema Guardiola.

"Tumezungumza na klabu na hisia zangu ni kwamba nataka kubaki sasa. Nitasalia msimu ujao na wakati wa msimu tutazungumza. Lakini baada ya miaka nane au tisa, tutaona."

Guardiola sasa ameshinda mataji 15 makubwa ndani ya miaka nane akiwa na City na anaweza kufikisha 16 kwa fainali ya Kombe la FA dhidi ya Manchester United wikendi ijayo.

Kocha huyo wa zamani wa Barcelona na Bayern Munich alikiri kuwa "amechoka" na akasema atahitaji kupata "motisha" mpya katika msimu wa majira ya joto kabla ya kuanza msimu mpya Agosti.

"Nina mkataba, bado nipo," alisema.

"Baadhi ya nyakati nina uchovu kidogo, lakini baadhi ya wakati ninaopenda na tuko hapa kushinda michezo, tukionekana vizuri tukiwa na wachezaji wapya.

"Ninaanza kufikiria, 'Hakuna aliyeshinda mara nne mfululizo, kwa nini tusijaribu?' Na sasa ninahisi imekamilika, kwa hivyo ni nini kinachofuata?

"Kwa sasa sijui ni nini hasa motisha ya kufanya hivyo kwa sababu ni vigumu kuipata wakati kila kitu kimekamilika."

Iwapo Guardiola atafuata ahadi yake ya kusalia City msimu ujao, anatarajia Arsenal itawania tena taji hilo.

Timu ya Mikel Arteta imemaliza ya pili katika kampeni mbili zilizopita baada ya kujikusanyia pointi 89 muhula huu. Guardiola alisema "amepata ujumbe."

"Hapo awali, ilikuwa Liverpool kuvuka mipaka yetu, na sasa ilikuwa Arsenal," Guardiola alisema.

"Nataka kuwapongeza kutoka ndani ya moyo wangu, kwa Mikel, wafanyakazi wake na wachezaji. Wamekuwa na msimu mzuri sana.

"Najisikia na wanatusukuma kwa ubora wetu kama hapo awali. Tulipata ujumbe kutoka kwa Mikel na wachezaji wake.

Inabidi tufanye maamuzi sahihi katika miaka ijayo kwa sababu wapo hapa kupambania mataji."

# Arteta awapoza mashabiki

**LONDON,** England

MIKEL Arteta ameitaka Arsenal kutoridhika kuwa washindi wa pili na ametaka kuendelea kuungana ili kushinda Ligi Kuu England baada ya kupata maumivu ya moyo kwa msimu wa pili mfululizo.

Washikabunduki hao walitoka nyuma na kuwalaza Everton 2-1 kwenye Uwanja wa Emirates kupitia mabao ya Takehiro Tomiyasu na Kai Havertz, lakini matokeo hayakutosha kwani Manchester City iliilaza West Ham 3-1 na kutwaa ubingwa kwa tofauti ya pointi mbili.

Akiwahutubia mashabiki waliofurika uwanjani, Arteta alisema: "Sasa ni wakati wa kuwa na mapumziko, kufikiria, kutafakari, na tafadhali endelea kusukuma. Endelea kuhamasisha timu hii. Usiridhike kwa sababu tunataka mengi zaidi ya hayo na tunakwenda kuipata."

Baadaye alipoulizwa kwa nini anajiamini hivyo, Arteta alijibu: "Ikiwa tutafanya kile tunachopaswa kufanya, tutakuwa karibu na mwisho tutashinda. Lini, sijui. Lakini ikiwa tutaendelea hivi, ninaamini mwishowe itatokea."

Arsenal ilimaliza msimu ikiwa na pointi 89 ikiwa timu tatu kumaliza kwa pointi nyingi kwenye msimu katika historia ya Ligi Kuu England.

Alipoulizwa kama City wamepandisha daraja la juu kiasi cha kuhitajika pointi 100 sasa, Arteta, ambaye alitumia miaka mitatu kama kocha chini ya Pep Guardiola kwenye Uwanja wa Etihad, alisema: "Ndio. Lakini nilikuwapo tulipofikisha pointi 100 hivyo kujua nini inachukua. Mimi najua nini kilitokea na hii ni ngazi."



HABARI MICHEZO

# SIMBA KUKOLEZA VITA NAFASI YA PILI LIGI KUU

**Na Faustine Feliciane**

KOCHA wa Simba, Juma Mgunda (pichani), amesema kuwa licha ya ugumu wa mchezo wa leo dhidi ya Geita Gold FC, bado malengo yao ni kuipata nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Simba kesho itakuwa mwenyeji wa Geita Gold FC kwenye uwanja wa Azam Complex katika mchezo wa mzunguko wa 28 huku ligi hiyo ikielekea ukingoni.

**Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Mgunda alisema wanaiheshimu Geita Gold kwa kuwa nao wana malengo yao kwenye mchezo huo lakini wamejiandaa vizuri kuwakabili.**

"Geita ni timu nzuri, bila kuangalia wapo katika nafasi ya ngapi, najua watapambana kutaka pointi tatu ndio sababu nasema hautakuwa mchezo mwepesi, pamoja na yote tumejiandaa vizuri kuwakabili," alisema Mgunda.

Alisema kuwa ana matumaini ya kufanya vizuri na amewataka wachezaji wake kutowadharau wapinzani wao.

"Lakini kingine kikubwa, nawaomba mashabiki waje kwa wingi, shabiki ni mchezaji wa 12, siku zote ana nafasi yake kwenye ushindi wa timu, natarajia watajitokeza kesho (leo) kama ilivyo kawaida," alisema Mgunda.

Simba inasaka kumaliza ligi katika nafasi ya pili ili kupata nafasi ya kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, nafasi hiyo wanachuana vikali na Azam FC ambao wote wanalingana kwa kuwa na pointi 60 baada ya kucheza michezo 27.






Mchezaji wa Timu ya Netiboli Wanawake ya JKT, Amina Abdul, akimiliki mpira huku akizongwa na wachezaji wa Timu ya NIC ya Uganda katika michuano ya ubingwa wa Afrika Mashariki mwishoni mwa wiki Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Yanga yaandaa 'surprise' sherehe za ubingwa Bara

INATOKA UKURASA 24

Alisema siku ya kukabidhiwa kombe lao itakuwa siku ndefu yenye furaha ambapo mashabiki watatamba na kuvimba kwa sababu ni siku ya mabingwa.

Aliongeza kuwa wamepeleka maombi serikalini na Bodi ya Ligi kuomba kuutumia Uwanja wa Benjamin Mkapa kucheza mchezo huo na kukabidhiwa kombe lao.

"Siku hiyo tutakuwa na burudani mbalimbali, tayari tiketi zimeanza kuuzwa, baada ya utaratibu wa mchezo kumalizika shughuli za sherehe zitaendelea hadi asubuhi," alisema Kamwe.

"Tumepanga kuondoka uwanjani hapo Jumapili Mei 26 na kulipeleka kombe letu makao makuu ya klabu, tutatumia njia ya Temeke mpaka Kariakoo, tukifika pale Msimbazi tutasimama kidogo na baadaye kuendelea na safari mpaka klabuni kwetu," alisema Kamwe.

## Morocco afurahia kiwango

INATOKA UKURASA 24

Aliongeza wachezaji hao wakiaminiwa na kupata uzoefu wa mechi za kimataifa, watakuwa ni nyota wa kutegemewa katika siku za baadaye kwa sababu hali ya kucheza kwa woga itawaondoka.

"Tukiwapa mechi nyingi na mechi hizo zikiwa za nje itakuwa jambo zuri katika mipango ya kuwaendeleza, pia tuwaamini, hii itawasaidia kuwajenga, wamekuwa tofauti katika mechi ya pili, wameanza kucheza kwa kuelewana," aliongeza kusema Morocco.

Kikosi hicho kinajiandaa kurejea nyumbani baada ya kumaliza michezo miwili ya kirafiki dhidi ya Sudan.

Morocco alilazimika kuita wachezaji wengi wapya na chipukizi kutokana na nyota wakongwe kubanwa na ratiba ya michezo ya kumaliza msimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya Kombe la FA ambayo hatua ya nusu fainali imemalizika juzi.

## *Biashara Utd mguu mmoja Ligi Kuu*

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Biashara United tayari imetanguliza mguu mmoja kurejea kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya juzi kuibuka na ushindi wa mabao 2-0 kwenye Uwanja wa Karume, Musoma dhidi ya Mbeya Kwanza kwenye mchezo wa kwanza wa 'Play off'.

Biashara iliyoshuka daraja msimu wa 2021/22 sasa itasubiri mechi ya marudiano itakayochezwa Jumapili ijayo, Uwanja wa Nangwanda Sijaona, Mtwara, kujua kama watarejea Ligi Kuu.

Timu inatakiwa kulinda ushindi wake huo kwa kulazimisha sare yoyote, au kupoteza mechi kwa idadi isiyozidi bao 1-0 ili kusonga mbele.

Kwa upande wa Mbeya Kwanza ambayo nayo ilishuka kutoka Ligi Kuu msimu wa 2021/22, italazimika kupata ushindi wa mabao 3-0 nyumbani ili kupita hatua hiyo.

Mabao ya Biashara juzi yalifungwa na Abeid Athumani na Boban Zirintusa.

Biashara United na Mbeya Kwanza zililazimika kucheza michezo ya 'Play Off', baada ya kumaliza nafasi ya tatu na ya nne katika Ligi ya 'Championship'.

Mbeya Kwanza ilimaliza nafasi ya tatu na pointi zake 65, Biashara United ikiwa ya nne ilikusanya pointi 62, huku ikiziacha timu za Ken Gold na Pamba zikipanda Ligi Kuu moja kwa moja.

# Michezo

Jumanne Mei 21, 2024

Nipashe




Usyk amchapa Fury

UKURASA 22




Wachezaji wa Manchester City wakishangilia kombe lao baada ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya England kwa mara ya nne mfululizo Jumapili, City iliifunga West Ham mabao 3-1 kwenye mchezo wa mwisho. **PICHA: MTANDAO**

# *Yanga yaandaa 'surprise' sherehe za ubingwa Bara*

**Saada Akida**

●●● Mabingwa hao kukabidhiwa kombe lao Mei 25 baada ya mchezo dhidi...

MABINGWA wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga wameandaa 'surprise' kwa mashabiki wao wakati wa sherehe za kukabidhiwa kombe la ubingwa huo, Mei 25 jijini Dar es Salaam.

Kikosi cha Yanga kimerejea jana kutoka Arusha, leo wanaelekea Dodoma kwa ajili ya mchezo dhidi ya Dodoma Jiji FC kabla ya kurejea Dar es Salaam kukabiliana na Tabora United. Akizungumza na Nipashe jana, ofisa habari wa klabu hiyo, Ali Kamwe, alisema siku hiyo ya mechi dhidi ya Tabora United itakuwa na mambo mengi mazuri kwa ajili ya mashabiki wao na watafanyia 'surprise' kubwa Wanayanga kabla ya kuanza kwa mchezo huo saa 10:00 jioni.



Ali Kamwe

**Alisema mchezo dhidi ya Dodoma FC utakuwa maalum kulishukuru benchi la ufundi kwa kazi nzuri na wameipa jina siku hiyo na kuiita 'Gamondi Day'.**

"Katika mchezo huu, ikifika dakika ya 30 mashabiki tutawaomba wasimame na kupiga makofi kulipongeza benchi letu la ufundi kwa kufanikisha ubingwa wetu wa 30.

"Alhamisi tunaenda bungeni baada ya kupata mwaliko kutoka Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo kusikiliza hotuba za bajeti zinazoendelea, baada ya hapo tunarejea Dar es Salaam kwa ajili ya maandalizi ya mchezo wa Mei 25, tumeomba mechi hii tukabidhiwe kombe letu la ubingwa," alisema Kamwe.

INAENDELEA UKURASA 23

## Morocco afurahia kiwango nyota wapya Taifa Stars

**Na Somoe Ng'itu**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Hemed Morocco, amefurahishwa na kiwango kilichoonyeshwa na wachezaji wa timu hiyo katika mechi mbili za kimataifa za kirafiki zilizofanyika nchini Saudi Arabia.

Morocco amesema hayo baada ya Stars kumaliza kwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Sudan katika mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa King Fahad ulioko Taif, nchini humo.

Kocha huyo alisema katika mechi ya juzi wachezaji wake walibadilika na kuonyesha kiwango bora huku kila mmoja akijituma.

Alisema anaamini wachezaji hao wakipata mechi zaidi za kirafiki wataimarika na kuwa msaada zaidi katika kikosi cha timu hiyo.

"Ilikuwa ni mechi nzuri na ngumu, wachezaji wangu walianza taratibu lakini walibadilika kadri muda ulivyokuwa unasogea, waliamka na hatimaye kupata bao la kusawazisha," alisema kocha huyo.




INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >